ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *2024/25*

GAVANA

BENKI KUU YA TANZANIA

Juni 2024

ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *2024/25*

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2024

11 Juni 2024

**Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb)**
**Waziri wa Fedha**
**Mji wa Serikali-Mtumba**
**Barabara ya Hazina**
**S. L.P 2802**
**40468 Dodoma**

Mheshimiwa Waziri,

**BARUA YA WASILISHO**

Kwa mujibu wa kifungu namba 21(3) hadi (6), cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, nawasilisha kwako ***Tamko la Sera ya Fedha*** kwa mwaka 2024/25, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Tamko hili la Sera ya Fedha linaainisha malengo na kutathmini matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2023/24. Aidha, Tamko hili linatathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini kwa mwaka 2023/24 na kuainisha mwelekeo wake kwa mwaka 2024/25. Vilevile, Tamko hili linabainisha mwelekeo wa sera ya fedha utakaotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2024/25 ili kufikia malengo ya sera ya fedha ya kudhibiti mfumuko wa bei na kukuza uchumi, pamoja na sera za riba na ubadilishaji wa fedha za kigeni zitakazotekelezwa kuendana na mfumo wa sera ya fedha.

Wasalaam,

Emmanuel M. Tutuba
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

# YALIYOMO


**BARUA YA WASILISHO** .................................................... **i**

**Muhtasari** .................................................... **v**

**SEHEMU YA KWANZA** .................................................... **1**

1.0 UTANGULIZI .................................................... 1

**SEHEMU YA PILI** .................................................... **4**

2.0 MALENGO YA SERA ZA KIUCHUMI NA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24 .................................................... 4

2.1 Malengo ya Sera za Kiuchumi .................................................... 4

**SEHEMU YA TATU** .................................................... **6**

3.0 UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24 .................................................... 6

**SEHEMU YA NNE** .................................................... **15**

4.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA .................................................... 15

**SEHEMU YA TANO** .................................................... **21**

5.0 MWENENDO WA UCHUMI WA NDANI .................................................... 21

5.1 Uchumi wa Tanzania Bara .................................................... 21

5.2 Uchumi wa Zanzibar .................................................... 37

**SEHEMU YA SITA** .................................................... **44**

6.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI .................................................... 44

6.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia .................................................... 44

6.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani .................................................... 45

**SEHEMU YA SABA ........................................................................ 48**

7.0 MWELEKEO WA SERA YA FEDHA, RIBA NA UBADILISHAJI FEDHA ZA KIGENI KWA MWAKA 2024/25............................ 48

7.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha ................................................ 48

7.2 Sera ya Riba ......................................................................... 49

7.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni ................................................................... 49

VIAMBATISHO ........................................................................... 50

# Muhtasari

## Malengo na matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Fedha

Katika kipindi cha mwaka 2023/24, sera ya fedha ililenga kuhami uchumi wa Tanzania dhidi ya athari za misukosuko ya uchumi wa dunia na ile ya ndani ya nchi, ili kuendelea kuwa na utulivu wa bei na ukuaji endelevu wa shughuli za kiuchumi. Katika kutimiza adhma hii, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha ya kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwa kutumia mfumo wa ujazi wa fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, ili kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yalikuwa ya kuridhisha. Ukwasi katika uchumi ulibaki katika viwango vya kuridhisha, kuendana na mahitaji ya uchumi, ambapo ujazi wa fedha na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa sambamba na malengo. Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha uliwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika programu ya IMF ya *Extended Credit Facility* (ECF) inayotekelezwa na Serikali.

Katika nusu ya pili ya mwaka 2023/24, Benki Kuu ilipanga kuhamia rasmi katika mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR)[1], kwa lengo la kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Hivyo basi, mwezi Januari 2024, Benki Kuu ilianza kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ya Benki Kuu (CBR) ambapo kupitia mfumo huu mpya na kwa kuzingatia maoteo ya mfumuko wa bei sambamba na mwenendo wa hali ya uchumi, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) iliamua riba ya Benki Kuu ya asilimia 5.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2024. Riba hiyo iliongezwa hadi asilimia 6 mwezi

1 Mabadiliko ya CBR yanatoa mwelekeo wa sera ya fedha, na riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki inatumika kama lengo la uendeshaji (*operating target*)

Aprili 2024 ili kudhibiti athari za hivi karibuni za kushuka kwa thamani ya shilingi kwenye mfumuko wa bei. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba ya Benki Kuu ulikuwa wa kuridhisha na ulifanikiwa kuhakikisha kuwa riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki inakuwa tulivu, ndani ya wigo usiozidi asilimia 2 chini au juu (+/-2) ya riba ya Benki Kuu. Vilevile, malengo yaliyowekwa katika programu ya ECF yalifikiwa.

Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha kwa mwaka 2023/24, kufikia takriban dola za Marekani bilioni 5, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa zaidi ya miezi 4. Hata hivyo, thamani ya shilingi dhidi ya sarafu mbalimbali duniani ilikumbana na changamoto zilizotokana na kupungua kwa fedha za kigeni katika soko la fedha za kigeni nchini hususan dola ya Marekani. Hali hii ilichangiwa na uamuzi wa benki kuu za nchi zilizoendelea kupandisha riba ili kukabiliana na mfumuko wa bei na ongezeko kubwa la mahitaji ya dola yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta ya nishati katika soko la dunia. Aidha, kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kulichangia ongezeko la mahitaji ya fedha za kigeni. Benki Kuu ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo, ikiwemo kuongeza mauzo ya fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni, kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi, kuondoa vikwazo vya kimasoko ili kuhakikisha kuwa bei inaakisi uwiano kati ya ugavi na mahitaji ya fedha za kigeni katika soko, na kushirikisha wadau kuhusu matumizi sahihi ya fedha za kigeni. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa asilimia 11.2 kwa mwaka unaoishia Aprili 2024, ikilinganishwa na kupungua kwa takriban asilimia moja katika miaka miwili iliyopita.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliimarika mwaka 2023/24, japo kwa kasi ndogo. Hali hii imetokana na benki kuu za nchi zilizoendelea kutekeleza sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei, migogoro ya kisiasa duniani na mabadiliko ya tabianchi. Mfumuko wa bei ulipungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa katika soko la dunia. Licha ya kupungua, kiwango cha mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea kilibaki juu ya malengo ya benki kuu za nchi hizo. Mfumuko wa bei katika nchi zinazoibukia kiuchumi umeendelea kupungua. Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya malengo ya kikanda katika nchi nyingi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Bei za bidhaa nyingi katika soko la dunia zilipungua hasa kuelekea mwishoni mwa mwaka 2023/24. Bei za mafuta ya nishati zimekuwa zikibadilika mara kwa mara, kutokana na migogoro ya kisiasa duniani na maamuzi ya uzalishaji ya umoja wa nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani (OPEC+). Aidha, bei ya dhahabu ilibaki juu kutokana na matarajio ya kupungua kwa riba za benki kuu na maamuzi ya benki kuu mbalimbali duniani kuanza kuweka dhahabu kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni hususan katika kipindi ambacho dunia inakabiliwa na changamoto za kiuchumi.

## Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

Ukuaji wa uchumi uliimarika katika mwaka 2023/24. Uchumi wa Tanzania Bara, ulikua kwa asilimia 5.1 mwaka 2023, ikilinganishwa na makadirio ya asilimia 5. Aidha, shughuli zilizochangia ukuaji huu ni kilimo, ujenzi na uchimbaji wa madini. Shughuli za utalii ambazo zinategemeana na sekta nyingine za uchumi zilichangia kwa kiasi

kikubwa ukuaji huo. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2022, kutokana na ongezeko la shughuli za huduma za malazi na chakula, hususan zinazohusiana na utalii, ikifuatiwa na ujenzi, upangishaji wa majengo na mazao.

Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara uliendelea kuwa tulivu, chini ya lengo la nchi la asilimia 5, kuendana na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya EAC na SADC. Mwenendo wa mfumuko wa bei ulichangiwa zaidi na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, na kushuka kwa bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei umeendelea kupungua, licha ya kuwa juu kidogo ya lengo la asilimia 5.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulikuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, mapato ya ndani kwa Tanzania Bara yalikuwa asilimia 94.1 ya makadirio. Aidha, mapato ya kodi yalikuwa asilimia 97.6 ya lengo. Mwenendo huu wa kuridhisha unaendana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini, na juhudi za Serikali kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari pamoja na kuboresha usimamizi wa kodi. Aidha, Serikali imeendelea kupanga matumizi kulingana na mapato. Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya ndani yalikuwa sawa na asilimia 99.7 ya lengo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024. Mapato ya kodi yalizidi lengo kwa asilimia 2.9, wakati mapato yasiyo ya kodi yalikuwa asilimia 80.3 ya lengo. Matumizi yaliwiana na mapato. Deni la Taifa limeendelea kuwa himilivu kwa mujibu wa vigezo vya upimaji vinavyokubaliwa kimataifa.

Sekta ya nje iliendelea kuimarika ukilinganisha na mwaka 2022/23, licha ya athari za mitikisiko ya kiuchumi duniani. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (*current account deficit*) ilipungua kwa kiasi kikubwa hadi dola za Marekani milioni 1,908.2 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,407.2 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi yatokanayo na utalii, dhahabu, na bidhaa asilia pamoja na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa Zanzibar, ziada ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 484.6 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 396.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikichangiwa zaidi na ongezeko la mapato yatokanayo na huduma hususan utalii.

Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara na thabiti. Sekta ya kibenki—ambayo ni sehemu kubwa ya sekta ya fedha— imeendelea kuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha na yenye kutengeneza faida. Sekta hii imeendelea kutumia teknolojia katika kutoa huduma za kifedha nchini, na hivyo kuchagiza ongezeko la amana na rasilimali. Ubora wa rasilimali za mabenki umeendelea kuongezeka ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.3 kwa mwezi Aprili 2024 kutoka asilimia 5.3 mwezi Juni 2023. Kupungua kwa mikopo chechefu kunatarajiwa kuendelea kuchagiza ongezeko zaidi la mikopo kwa sekta binafsi. Mifumo ya malipo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi, na kuwezesha utekelezaji wa sera ya fedha na kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Benki Kuu imeendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya malipo ili kuongeza ufanisi. Aidha, simu za mkononi zimeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kuwawezesha wananchi wasio na akaunti benki kupata huduma za kifedha.

**Matarajio ya Hali ya Uchumi**

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kuimarika kwa mwaka 2024 na 2025, kutokana na kupungua kwa vikwazo vya ukuaji vilivyoikumba dunia baada ya janga la UVIKO-19. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), linakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2024 na 2025. Makadirio haya yanatokana na matarajio ya benki kuu za nchi zilizoendelea kuanza kupunguza riba za sera ya fedha sambamba na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Aidha, matarajio hayo yatategemea mabadiliko ya bei za nishati, migogoro ya kisiasa na maamuzi ya benki kuu za nchi zilizoendelea kuhusu mwelekeo wa riba katika kutekeleza sera ya fedha. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi, na kutengemaa kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa duniani. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua kwa kasi hadi kufikia lengo la asilimia 2 ukilinganisha na nchi zinazoibukia kiuchumi, na kusababisha nchi hizo kuanza kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi. Mwenendo huu wa mfumuko wa bei utategemea migogoro ya kisiasa duniani na maamuzi ya kiwango cha uzalishaji ya umoja wa nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani (OPEC+).

Uchumi wa Tanzania, unatarajiwa kuendelea kuimarika, sambamba na kutengemaa kwa mazingira ya kiuchumi duniani na nchini. Uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 5.8 mwaka 2025, ukichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, uchimbaji madini na utalii. Ukuaji katika sekta ya kilimo utachagizwa na matarajio ya kuwepo kwa mvua za kutosha nchini pamoja na utekelezaji wa sera mbalimbali zinazolenga kuchochea uzalishaji katika sekta ya kilimo na mnyororo mzima wa uzalishaji katika sekta hii. Ukuaji katika shughuli za ujenzi unategemea uwekezaji

unaondelea kufanyika katika miundombinu, wakati kuimarika kwa sekta ya madini kunategemea ongezeko la uzalishaji katika migodi iliyopo na uwekezaji mpya katika uchimbaji wa madini na ongezeko la bei katika soko la dunia. Ukuaji katika shughuli za utalii utachangiwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali kuinua sekta hii ikiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji, kuhamasisha na kuvutia watalii kutoka nchi mbalimbali. Uchumi wa Zanzibar, unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2024 na 6.8 mwaka 2025, ukichangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na viwanda. Mwenendo huu wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar unaakisi matarajio ya kukamilika kwa miradi mikubwa ya ujenzi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, uhakika wa upatikanaji wa umeme na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

**Mwelekeo wa Sera ya Fedha kwa Mwaka 2024/25**

Katika mwaka 2024/25, sera ya fedha inalenga kuendelea kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 na kuwezesha ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 5.8 mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na asilimia 7.2 na asilimia 6.8 kwa Zanzibar. Mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 ni kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi ili kukabiliana na athari za hivi karibuni zinazotokana na kushuka kwa thamani ya shilingi kwenye mfumuko wa bei. Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR), ambayo itafanyiwa mapitio kila robo mwaka. Aidha Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu.

## Sera ya Riba

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko. Mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, utaendelea kuchangia katika kuwezesha taasisi za fedha kupanga riba kwa kuzingatia nguvu ya soko. Hivyo basi, riba ya Benki Kuu (CBR), itatumika kama kigezo kimojawapo katika ukokotoaji wa viwango vya riba. Hii itaenda sambamba na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika kutekeleza maboresho katika sekta ya fedha, kuboresha jitihada za kumlinda mlaji, kutoa elimu ya masuala ya fedha na huduma jumuishi za kifedha.

## Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni

Viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni vitaendelea kuamuliwa na nguvu za soko, ikiwa ni njia ya msingi ya kuzuia madhara ya mitikisiko ya uchumi toka nje ya nchi. Benki Kuu itaendelea kufuatilia na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya mabenki (IFEM) kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki katika Soko la Fedha za Kigeni (*Foreign Exchange Intervention Policy*) na kuhakikisha washiriki wanafuata kanuni za maadili ya IFEM (*IFEM code of conduct*). Aidha, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ili iweze kutumika kama kinga dhidi ya mitikisiko ya kiuchumi kutoka nje ya nchi.

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, lengo la msingi la Benki Kuu ni kubuni, kuandaa, na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei ili kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya ukuaji endelevu wa uchumi. Vilevile, Kifungu cha 7(2) cha Sheria hiyo kinaielekeza Benki Kuu, kuhakikisha uthabiti wa sekta ya fedha, kusaidia utekelezaji wa sera za kiuchumi za Serikali, pamoja na kuchagiza mazingira wezeshi ya kifedha, ikiwemo upatikanaji wa mikopo kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa kwa ujumla, bila kuathiri lengo la utulivu wa bei. Aidha kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Kifungu 21(3) hadi (6), sura 197, Benki Kuu ya Tanzania inatakiwa kutoa **Tamko la Sera ya Fedha** mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka, mwezi Februari linalojumuisha uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha.

Tamko hili limeandaliwa kwa mtiririko ufuatao: Sehemu ya pili inafanya marejeo ya malengo ya sera za kiuchumi za Serikali kwa mwaka 2023/24, wakati Sehemu ya tatu inaainisha malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2023/24. Sehemu ya nne inachambua mwenendo wa uchumi wa dunia, ikifuatiwa na Sehemu ya tano inayotathmini mwenendo wa uchumi hapa nchini. Sehemu ya sita inatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini ikifuatiwa na Sehemu ya saba ambayo inatoa mwelekeo wa sera ya fedha pamoja na sera za riba na ubadilishaji wa fedha za kigeni zitakazotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kufikia malengo yake ya kisera kwa mwaka 2024/25 ambayo ni kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania**

Mfumo wa sera ya fedha ya Benki Kuu ya Tanzania hulenga kudhibiti mfumuko wa bei nchini na kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi. Mnamo mwezi Januari 2024, Benki kuu ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ili kuongeza ufanisi, sawia na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Mfumo huu ambao unazingatia zaidi mwelekeo na matarajio ya mwenendo wa viashiria mbalimbali vya kiuchumi (*forward looking*) hutumia Riba ya Benki Kuu ili kuchagiza mwenendo wa riba za muda mfupi katika masoko ya fedha, ambazo hutarajiwa kuashiria viwango vya riba vya muda mrefu na hatimaye kuathiri mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Mambo muhimu katika mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu yameainishwa kama ifuatavyo.

**Lengo la Sera ya Fedha**

Lengo la msingi la sera ya fedha ni kuhakikisha utulivu wa bei, yaani kiwango kidogo na thabiti cha mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya kila mwaka katika fahirisi za bei za walaji nchini ambalo huwasilishwa kwa asilimia. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa ndani ya wigo wa asilimia 3-5 katika muda wa kati. Lengo hili ni muafaka kwa ajili ya kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi nchini, pamoja na kuhakikisha utulivu wa riba na thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi nyingine.

**Lengo la Kati**

Benki Kuu inadhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi kwa kutumia kiwango cha riba ya Benki Kuu (CBR). Riba hii hupangwa kuendana na maoteo ya mfumuko wa bei, sambamba na ukuaji endelevu wa uchumi.

**Kiashiria cha Utendaji**

Chini ya mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, Benki Kuu inahakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki (lengo la uendeshaji) inaendana na riba ya Benki Kuu ili kufikia malengo ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki imechaguliwa na Benki Kuu kwa kuwa ni tulivu na ina uhusiano wa karibu na riba ya Benki Kuu.

**Nyenzo za Sera ya Fedha**

Benki Kuu ya Tanzania inatumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa lengo la uendeshaji linaendana na riba ya Benki Kuu. Nyenzo kuu za utekelezaji wa Sera ya fedha ni pamoja na Benki Kuu kuingia mikataba ya mauziano au manunuzi ya dhamana za muda mfupi na benki za biashara (*repurchase agreement and reverse repurchase agreement*). Nyenzo nyingine ni uuzaji na ununuzi wa dhamana (*debt securities*), na uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya mabenki. Nyenzo nyingine zinazotumika ni pamoja na kiwango cha amana za benki za biashara kinachotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu (*Statutory Minimum Reserve*) na riba inayotumika kutoza benki au Serikali zinapochukua mikopo Benki Kuu. Pamoja na nyenzo hizo, Benki Kuu pia inatoa mikopo ya muda mfupi ambayo hutakiwa kurudishwa ndani ya siku husika na ikijumuisha ya siku moja (*Intraday and Lombard loan facilities*). Aidha, Benki Kuu inaweza kutumia nyenzo nyingine za sera ya fedha kuendana na mahitaji ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya kisera.

**Uwasilishaji wa Sera ya Fedha kwa Umma**

Benki Kuu ya Tanzania inatekeleza jukumu lake la uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha kwa uwazi. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha, ikiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu inawasilishwa kwenye mkutano wa Gavana na wakuu wa taasisi za kibenki na pia kwa umma kupitia vyombo vya habari. Vilevile, Benki Kuu huandaa na kuchapisha Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha na taarifa mbalimbali zinazoainisha mwelekeo wa sera ya fedha, matokeo ya utekelezaji wake na mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Taarifa hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu.

**Utekelezaji wa Sera ya Fedha**

- Mwanzo wa kila mwaka wa fedha, Benki Kuu ya Tanzania hutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika Tamko lake la Sera ya Fedha kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.

- Tamko la Sera ya Fedha inaidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania na kuwasilishwa bungeni kupitia kwa Waziri anayesimamia masuala ya fedha.

- Utaratibu huo pia unafuatwa wakati ya uandaaji wa Mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, ambayo huainisha maendeleo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo yake, matarajio kwa kipindi cha mwaka kilichosalia, na hatua zitakazochukuliwa ili kufikia malengo ya sera.

- Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu, ambayo inaongozwa na Gavana, inawajibika kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kila robo mwaka, kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.

- Kamati ya Ufuatiliaji na Uangalizi ya Menejimenti ya Benki Kuu inakutana kila siku kutathmini mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki (kiashiria cha uendeshaji) na kuamua hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha riba hiyo inabaki ndani ya wigo unatakiwa.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MALENGO YA SERA ZA KIUCHUMI NA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24

### 2.1 Malengo ya sera za kiuchumi

Malengo ya sera za kiuchumi kwa mwaka 2023/24 yalikuwa ni: kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 5 kwa mwaka 2023 na asilimia 5.5 kwa mwaka 2024 kwa Tanzania Bara na ukuaji wa asilimia 7.1 na asilimia 7.4, kwa Zanzibar, na kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 5 kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Malengo haya yalipangwa sanjari na miongozo ya maendeleo ya Taifa, yaani Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026. Malengo haya pia yalizingatia mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Hata hivyo, uchumi wa dunia ulikumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo migogoro ya kisiasa, mazingira magumu ya upatikanaji mitaji na fedha, na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, uchumi wa ndani ulikabiliwa na upungufu wa ukwasi wa fedha za kigeni na nishati.

Ili kufikia malengo ya kiuchumi, sera ya fedha ilijikita katika kuhami uchumi dhidi ya mitikisiko iliyoukumba uchumi wa dunia na hapa nchini. Hivyo basi, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, Benki Kuu ililenga kutekeleza sera ya fedha ya kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi kwa kutumia mfumo wa ujazi wa fedha. Malengo ya sera ya fedha yalikuwa ni: (i) ukuaji wa fedha taslimu (M0) wa asilimia 10.1; (ii) ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) wa asilimia 10.1; na (iii) ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 16.4.

Aidha katika nusu ya pili ya mwaka 2023/24, Benki Kuu ilipanga kuhamia rasmi katika mfumo wa utekelezaji wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR)[2], kwa lengo la kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Vilevile, utekelezaji wa sera chini ya mifumo yote miwili ulilenga kuendelea kuhakikisha kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne na kufikiwa kwa vigezo vilivyoainishwa kwenye programu ya IMF ya *Extended Credit Facility (ECF)* inayotekelezwa na Serikali.


2 Mabadiliko ya CBR yanatoa mwelekeo wa sera ya fedha, na riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya mabenki inatumika kama lengo la uendeshaji (*operating target*)

# SEHEMU YA TATU

## 3.0 UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24


Matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha yalikuwa ya kuridhisha, licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan zilizotokana na mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, Benki Kuu ilitekeleza sera ya fedha ya kupunguza kasi ya ongezeko la ukuaji wa ukwasi katika uchumi kwa kutumia mfumo unaolenga ujazi wa fedha. Lengo la utekelezaji wa sera hii lilikuwa ni kudhibiti mfumuko wa bei kutokana na mitikisiko ya kiuchumi na kuendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za uzalishaji nchini. Utekelezaji wa sera ya fedha uliweza kufikia malengo yaliyokusudiwa ambapo, kiwango cha ukwasi katika uchumi kilitosheleza mahitaji ya shughuli za uzalishaji nchini na kuwezesha benki kutoa mikopo kwa sekta binafsi. Ukuaji wa viashiria vya ujazi wa fedha ulienda sawia na malengo, ambapo katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, ukuaji wa fedha taslimu (M0) na ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa takriban asilimia 15.5 na asilimia 5.6, mtawalia (Kielelezo 3.1a). Wakati huo huo, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa wastani wa asilimia 19.1, ukilinganisha na lengo la asilimia 16.4 (Kielelezo 3.1b).

## Kielelezo 3.1a: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 3.1b: Ukuaji wa Mikopo kwa Sekta Binafsi





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Mnamo mwezi Januari 2024, Benki Kuu ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ya Benki Kuu (CBR), lengo ikiwa ni kuongeza ufanisi wa sera ya fedha ili kuendana na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia riba


ya Benki Kuu ulikuwa wa kuridhisha kutokana na maandalizi mazuri na kushirikisha wadau katika kutumia mfumo huu mpya. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kupitia Mkutano wake wa Januari 2024, iliamua riba ya Benki Kuu ya asilimia 5.5 kwa kuzingatia maoteo ya mfumuko wa bei sambamba na mwenendo wa hali ya uchumi, ambayo ilitumika kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024. Riba hiyo iliongezwa hadi asilimia 6 mwezi Aprili 2024 ili kudhibiti mfumuko wa bei kutokana na athari za kushuka kwa thamani ya shilingi katika kipindi cha hivi karibuni. Kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia mfumo huu mpya, riba katika soko la fedha baina ya mabenki zilikuwa tulivu, ndani ya wigo usiozidi asilimia 2 chini au juu (+/-2) ya riba ya Benki Kuu katika kipindi cha Januari hadi Mei 2024 (Kielelezo 3.1d).

**Kielelezo 3.1c: Amana za Mabenki na Riba za Mikopo Baina ya Mabenki**




*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

## Kielelezo 3.1d: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa imara, licha ya kasi ya ongezeko kupungua. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 17, ukilinganisha na asilimia 22.9 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi lilichangiwa zaidi na mikopo iliyoelekezwa kwenye shughuli binafsi, kilimo na uzalishaji viwandani (Kielelezo 3.1e). Sehemu kubwa ya mikopo ya shughuli binafsi ilielekezwa katika biashara na shughuli ndogo ndogo na za kati ambazo kwa kiwango kikubwa zinamilikiwa na wafanyabiashara wadogo na wa kati[3] (Kielelezo 3.1f). Mahitaji ya mikopo yanatarajiwa kuendelea kuongezeka kufuatia utekelezaji wa sera wezeshi, kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi duniani na nchini pamoja na maboresho katika mazingira ya kibiashara nchini.

3 Mikopo ya shughuli binafsi inatolewa kwa biashara ndogo na za kati. Mikopo hii inapendelewa zaidi kwa sababu ya upatikanaji rahisi, masharti nafuu ya dhamana, na baadhi hutumia mishahara kama dhamana.

## Kielelezo 3.1e: Mchango wa Shughuli za Uchumi Katika Ukuaji wa Mikopo


Asilimia




*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 3.1f: Sehemu ya Mikopo kwa Jumla ya Mikopo

Asilimia





*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

Vilevile, utekelezaji wa sera ya fedha ulisaidia kufikiwa kwa vigezo vilivyoainishwa katika programu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya *Extended Credit Facility (ECF)* kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024.


Katika nusu ya kwanza ya 2023/24, riba za dhamana za serikali ziliongezeka kabla ya kuanza kupungua kuanzia nusu ya pili ya 2023/24 zikiakisi ukwasi wa kutosha kwenye uchumi (Kielelezo 3.2a). Aidha, riba za mikopo zilipungua katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2023/24 hadi wastani wa asilimia 16 (Kielelezo 3.2b). Mathalan, riba ya mikopo inayotolewa kwa wateja wakubwa ilipungua hadi asilimia 13 kutoka asilimia 14. Riba za amana ziliongezeka kidogo, hadi takriban asilimia 7, wakati riba za amana za wateja wakubwa zikiwa takriban asilimia 8. Riba za mikopo zinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto za kimuundo katika soko la fedha pamoja na uwepo wa mfumuko wa bei mdogo nchini.

**Kielelezo 3.2a: Riba za Mikopo Katika Masoko ya Fedha**




*Chanzo:* Uchambuzi wa mabenki na Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 3.2b: Riba za Mikopo na Amana za Mabenki**




*Chanzo:* Uchambuzi wa mabenki na Benki Kuu ya Tanzania


Akiba ya fedha za kigeni iliimarika. Hadi kufikia mwishoni mwa Mei 2024, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani milioni 5,162.6, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.3. Kiasi hiki ni ndani ya malengo na kiwango cha nchi cha angalau miezi 4 ya uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi[4] (Kielelezo 3.3).

Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilipungua kwa asilimia 11.2 kwa mwaka unaoishia mwezi Aprili 2024, ikilinganishwa na takriban asilimia moja kwa miaka miwili iliyopita (Kielelezo 3.4a). Hali hii ilichangiwa na uamuzi wa benki kuu za nchi zilizoendelea wa kupandisha riba katika kukabiliana na mfumuko wa bei na ongezeko kubwa la mahitaji ya dola yaliyotokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta ya nishati katika soko la dunia. Aidha, kulikuwa na ongezeko la mahitaji ya dola kutokana na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji na

4 Miezi ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi, huondoa baadhi ya bidhaa zinazoagizwa kwa ajili ya uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (Foreign Direct Investment)


biashara nchini. Benki Kuu ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo, ikiwemo kuuza sehemu ya akiba ya fedha za kigeni katika soko, utekelezaji wa sera ya fedha yenye kupunguza ukwasi na kushirikisha wadau kuhusu matumizi sahihi ya fedha za kigeni. Aidha kiwango halisi cha ubadilishaji fedha (*real effective exchange rate*) kimeendelea kuakisi mwenendo wa uchumi nchini (Kielelezo 3.4b).

**Kielelezo 3.3: Akiba ya Fedha za Kigeni**





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 3.4a: Mwenendo wa Kiwango cha Ubadilishaji Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 3.4b: Kiwango Halisi cha Ubadilishaji wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania
*Kumbuka:* R1 Robo ya kwanza

# SEHEMU YA NNE

## 4.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA

Uchumi wa dunia uliimarika mwaka 2023/24, licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea, migogoro ya kisiasa duniani, kuongezeka kwa bei za mafuta ya nishati, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Uchumi wa nchi zilizoendelea ulionesha uhimilivu, ukiakisiwa na ukuaji wa ajira na kipato, kufuatia kuongeza kwa mahitaji na ugavi wa bidhaa. Ukuaji wa uchumi kwa nchi nyingi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi uliimarika kwa mwaka 2023 (Jedwali 4.1). Vilevile, kwa upande wa nchi zilizopo kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi uliimarika licha ya changamoto za gharama kubwa za mikopo na uwezo mdogo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Hata hivyo, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi licha ya kubaki juu ya malengo ya benki kuu, hususan katika nchi zilizoendelea. Mfumuko wa bei wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kupungua hadi kufika kwenye malengo ya benki kuu ya nchi hizo mapema zaidi kuliko nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea (Kielelezo 4.1a). Katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulipungua hadi kufikia asilimia 6 mwaka 2023 kutoka asilimia 10 mwaka 2022 kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ongezeko la ukwasi pamoja na kupungua kwa bei za vyakula na nishati. Katika nchi nyingi za EAC na SADC, mfumuko wa bei ulipungua na kuwa ndani ya malengo ya kikanda (Kielelezo 4.1b na 4.1c).


## Jedwali 4.1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Robo Mwaka

*Asilimia*

| | Halisi | | | | Makadirio |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2023 | | | | 2024 |
| | Robo 1 | Robo 2 | Robo 3 | Robo 4 | Robo 1 |
| Marekani | 0.6 | 0.5 | 1.2 | 0.8 | 0.3 |
| Ukanda wa Euro | 0.1 | 0.1 | -0.1 | 0.0 | 0.2 |
| Japani | 2.0 | 4.2 | -3.2 | 0.4 | 0.2 |
| Uingereza | 0.1 | 0.0 | -0.1 | -0.3 | 0.2 |
| China | 2.1 | 0.6 | 1.5 | 1.0 | 1.3 |
| Afrika ya Kusini | 0.3 | 0.7 | -0.2 | 0.1 | 0.3 |


*Chanzo:* Bloomberg

## Kielelezo 4.1a: Mfumuko wa Bei kwa Nchi Zilizoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi




*Chanzo:* Ofisi za Takwimu za Nchi husika


## Kielelezo 4.1b: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za EAC




*Chanzo:* Ofisi za Takwimu za Nchi husika

## Kielelezo 4.1c: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi za Takwimu za Nchi husika

Bei za bidhaa katika soko la dunia zilipungua kwa kasi kubwa kuelekea mwishoni mwa mwaka 2023/24 ikilinganishwa na mwanzo wa mwaka (Kielelezo 4.2a na 4.2b). Ingawa bei za mafuta zilipungua, kulikuwa na ongezeko kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2024, kutokana na migogoro ya kisiasa, maamuzi ya OPEC+ kuhusu kiwango cha uzalishaji wa mafuta, na kuongezeka kwa mahitaji. Bei ya dhahabu ilibaki juu kutokana na matarajio ya kupungua kwa riba za benki kuu na maamuzi ya benki kuu mbalimbali duniani kuanza kuweka dhahabu kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni hususan kunapokuwa na changamoto za kiuchumi.


Nchi nyingi zilizoendelea zimeendelea kutekeleza sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika uchumi, ambapo riba za benki kuu ziliendelea kuwa juu. Kutokana na hali hii, gharama za mikopo ziliendelea kuwa kubwa huku masharti ya upatikanaji wa fedha yakiendelea kuwa magumu katika nchi nyingi. Hata hivyo, benki kuu za nchi zilizoendelea zinatarajiwa kuanza kupunguza riba za sera za fedha ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Mathalani, Benki Kuu ya Umoja wa Ulaya inatarajiwa kuanza kushusha riba yake kuanzia Juni 2024 japo Benki Kuu ya Marekani inatarajiwa kuchelewa kidogo kupunguza riba yake. Matarajio ya kupungua kwa riba katika nchi zilizoendea, kunaweza kurahisisha upatikanaji wa mitaji katika nchi zinazoendelea.

**Kielelezo 4.2a: Bei za Bidhaa Zinazoingia Nchini**




*Chanzo:* Benki ya Dunia na Bloomberg

## Kielelezo 4.2b: Bei za Bidhaa Zinazotoka Nchini




*Chanzo:* Benki ya Dunia na Bloomberg

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 MWENENDO WA UCHUMI WA NDANI


## 5.1 Uchumi wa Tanzania Bara

### 5.1.1 Pato la Taifa

Shughuli za kiuchumi ziliimarika kwa mwaka 2023, ukilinganisha na mwaka uliopita kutokana na kuimarika kwa mazingira ya kibiashara, uwekezaji na sera wezeshi. Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 5.1, ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 4.7, na juu ya makadirio ya asilimia 5, likichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo, ujenzi, na uchimbaji madini (Kielelezo 5.1a na b). Shughuli za utalii ambazo zinategemeana na sekta nyingine za uchumi zilichangia kwa kiasi kikubwa ukuaji huo. Kwa upande wa shughuli zilizokua kwa kasi zaidi ni sanaa na burudani, fedha na bima, uchimbaji wa madini pamoja na malazi na huduma za chakula hususan zinazohusiana na utalii (Kielelezo 5.1c). Viashiria vya kiuchumi kwa robo mbili za mwanzo za mwaka 2024 vinaonesha kuendelea kuimarika kwa uchumi. Mwelekeo huu unatarajiwa kuendelea, kutokana na jitihada zinazoendelea za kuboresha mazingira ya biashara na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi.

## Kielelezo 5.1a: Pato la Taifa


*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Kielelezo 5.1b: Mchango wa Ukuaji


*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 5.1c: Ukuaji wa Shughuli za Kiuchumi**

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### 5.1.2 Mfumuko wa Bei


Mfumuko wa bei uliendelea kuwa tulivu na chini ya lengo la nchi la asilimia 5, kuendana na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi vya EAC na SADC vya mfumuko wa bei usiozidi asilimia 8 na kati ya asilimia 3-7, mtawalia (Kielelezo 5.2b). Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.2, ukipungua kutoka asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia (Kielelezo 5.2a). Kupungua huko kulisababishwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, uwepo wa chakula cha kutosha nchini, na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. Mfumuko wa bei ya chakula ulishuka hadi asilimia 3.4, kutoka asilimia 8.9 katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ya nishati, ulipungua kufikia wastani wa asilimia 4.1, kutoka asilimia 7.2, ukiakisi mwenendo wa bei za bidhaa za petroli katika soko la dunia. Hata hivyo, mfumuko wa bei wa msingi (*core inflation*) uliongezeka kidogo na kufikia wastani wa asilimia 3 kutoka asilimia 2.7 (Kielelezo 5.2c).

### Kielelezo 5.2a: Mfumuko wa Bei





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### Kielelezo 5.2b: Mfumuko wa Bei na Malengo ya Nchi na Kikanda




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 5.2c: Mchango katika Mfumuko wa Bei**




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### 5.1.3 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, utekelezaji wa bajeti ya Serikali uliendelea kuwa wa kuridhisha. Mapato ya ndani yanayojumuisha mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, yalikuwa asilimia 94.1 ya makadirio (Jedwali 5.1). Aidha, makusanyo ya kodi yalikuwa asilimia 97.6 ya lengo. Mwenendo huu ni matokeo ya juhudi za Serikali katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 29,544.7, ambapo asilimia 41.1 zilielekezwa katika miradi na shughuli za maendeleo.

**Jedwali 5.1: Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali**

*Shilingi bilioni*

| | Julai 2022-Aprili 2023 | Julai 2023-Aprili 2024 | | |
|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Makadirio | Halisi | Halisi/Makadirio (%) |
| Mapato | 21,666.2 | 25,658.1 | 24,148.2 | 94.1 |
| Matumizi | 27,941.1 | 32,456.2 | 29,544.7 | 91.0 |
| Matumizi ya kawaida | 16,298.4 | 19,898.3 | 17,401.8 | 87.5 |
| Matumizi ya maendeleo | 11,642.7 | 12,597.9 | 12,142.9 | 96.4 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

## 5.1.4 Deni la Taifa

Deni la Taifa limeendelea kuwa himilivu katika kipindi cha muda wa kati na mrefu, kwa kuwa na vihatarishi vya wastani[5] . Uwiano wa thamani (*Present Value*) ya deni la serikali kwa pato la taifa ilikuwa asilimia 30.8, dhidi ya ukomo wa asilimia 55. Deni la Serikali liliongezeka kwa asilimia 3.1 hadi dola za Marekani milioni 36,210.7 mwishoni mwa Aprili 2024, kutoka kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa Juni 2023. Ongezeko hili lilitokana na mikopo ya kugharamia miradi na shughuli za maendeleo.

Deni la nje lilikuwa sawa na asilimia 66.4 ya deni la Taifa (Jedwali 5.2a). Sehemu kubwa ya deni la nje la Serikali Kuu ilikuwa ni mikopo nafuu kutoka taasisi za kimataifa, ikifuatiwa na mikopo ya kibiashara (Jedwali 5.2b). Sehemu kubwa ya fedha zilizotokana na mikopo ya nje ilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo katika sekta za usafirishaji na mawasiliano, ikifuatiwa na huduma za jamii na elimu (Jedwali 5.2c). Deni la ndani la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 31,339.3 mwezi Aprili 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.3 kutoka mwezi Juni 2023, huku kiwango kikubwa kikiwa ni hati fungani.

Malipo ya deni la nje katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 yalikuwa dola za Marekani milioni 1,575.4, ambapo asilimia 85.3 ya malipo ililipwa na Serikali Kuu (Kielelezo 5.3a). Wakati huohuo, kiasi cha shilingi bilioni 5,075.5 kilitumika kulipa madeni ya ndani (Kielelezo 5.3b).

5 Matokeo haya ni kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa iliyofanyika Oktoba 2023

## Jedwali 5.2a: Deni la Taifa

*Dola milioni*

| | Jun-23 | Dis-23 | Apr-24[A] |
|---|---|---|---|
| Serikali kuu | 35,222.6 | 34,794.3 | 36,210.7 |
| Deni la nje | 22,794.3 | 22,552.3 | 24,029.1 |
| % ya deni la Serikali | 64.7 | 64.8 | 66.4 |
| Deni la ndani | 12,428.3 | 12,242.0 | 12,181.7 |
| Deni la nje la sekta binafsi | 7,425.2 | 9,169.8 | 9,080.6 |
| Deni la nje la mashirika ya umma | 33.2 | 11.8 | 12.8 |
| Jumla ya deni la nje | 30,252.7 | 31,733.9 | 33,122.4 |
| Jumla ya deni la Taifa | 42,681.0 | 43,975.9 | 45,304.1 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Kumbuka:* A inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 5.2b: Wadai wa Deni la Nje

*Dola milioni*

| | Jun-23 | | Dis-23 | | Apr-24[A] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkopeshaji | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Mashirika ya kimataifa | 14,724.0 | 48.7 | 15,430.5 | 48.6 | 16,712.2 | 50.5 |
| Deni ambalo halijalipwa | 14,663.3 | 48.5 | 15,307.9 | 48.2 | 16,589.4 | 50.1 |
| Malimbikizo ya riba | 60.7 | 0.2 | 122.6 | 0.4 | 122.8 | 0.4 |
| Nchi wahisani | 2,232.8 | 7.4 | 1,366.2 | 4.3 | 1,370.4 | 4.1 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,114.5 | 3.7 | 1,114.4 | 3.5 | 1,118.5 | 3.4 |
| Malimbikizo ya riba | 1,118.3 | 3.7 | 251.9 | 0.8 | 251.9 | 0.8 |
| Kibiashara | 8,817.3 | 29.1 | 12,259.1 | 38.6 | 12,341.7 | 37.3 |
| Deni ambalo halijalipwa | 8,053.4 | 26.6 | 11,099.6 | 35.0 | 11,180.5 | 33.8 |
| Malimbikizo ya riba | 763.9 | 2.5 | 1,159.5 | 3.7 | 1,161.1 | 3.5 |
| *Export credit* | 4,478.6 | 14.8 | 2,678.0 | 8.4 | 2,698.2 | 8.1 |
| Deni ambalo halijalipwa | 4,058.1 | 13.4 | 1,953.2 | 6.2 | 1,932.1 | 5.8 |
| Malimbikizo ya riba | 420.5 | 1.4 | 724.9 | 2.3 | 766.2 | 2.3 |
| Deni la nje | 30,252.7 | 100.0 | 31,733.9 | 100.0 | 33,122.4 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Kumbuka:* A inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 5.2c: Matumizi ya Mikopo ya Nje Iliyopokelewa

*Dola milioni*

| | Jun-23 | | Dis-23 | | Apr-24^A | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli ya uchumi | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Urari wa malipo na msaada wa bajeti | 2,954.0 | 10.6 | 3,730.3 | 12.7 | 5,220.3 | 16.9 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 5,604.2 | 20.1 | 6,580.7 | 22.3 | 6,682.4 | 21.7 |
| Kilimo | 1,482.0 | 5.3 | 1,527.9 | 5.2 | 1,509.0 | 4.9 |
| Nishati na madini | 4,225.6 | 15.2 | 4,479.4 | 15.2 | 4,562.1 | 14.8 |
| Viwanda | 1,443.2 | 5.2 | 1,381.5 | 4.7 | 1,371.6 | 4.5 |
| Huduma za jamii na elimu | 4,534.1 | 16.3 | 5,516.7 | 18.7 | 5,926.8 | 19.2 |
| Fedha na bima | 978.0 | 3.5 | 1,345.0 | 4.6 | 1,278.1 | 4.1 |
| Utalii | 409.3 | 1.5 | 473.8 | 1.6 | 486.9 | 1.6 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 2,218.3 | 8.0 | 1,745.0 | 5.9 | 1,675.8 | 5.4 |
| Mengineyo | 4,040.6 | 14.5 | 2,694.8 | 9.1 | 2,107.5 | 6.8 |
| Jumla | 27,889.3 | 100.0 | 29,475.0 | 100.0 | 30,820.4 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Kumbuka:* A inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 5.2d: Deni la Ndani


*Dola milioni*

| | Jun-23 | | Dis-23 | | Apr-24^A | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Dhamana za serikali | 24,682.3 | 85.3 | 26,072.4 | 85.0 | 26,678.6 | 85.1 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,129.2 | 7.4 | 2,730.6 | 8.9 | 2,632.7 | 8.4 |
| Hisa za serikali | 252.7 | 0.9 | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.6 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 22,300.2 | 77.1 | 23,154.6 | 75.5 | 23,858.7 | 76.1 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 4,244.8 | 14.7 | 4,606.4 | 15.0 | 4,660.7 | 14.9 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 |
| Bakaa hasi | 4,226.4 | 14.6 | 4,588.0 | 15.0 | 4,642.3 | 14.8 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 28,927.1 | 100.0 | 30,678.9 | 100.0 | 31,339.3 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Kumbuka:* *Inajumuisha mkopo wa kawaida wa benki ya biashara; na A inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 5.3a: Malipo ya Deni la Nje


*Dola milioni*




*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu

## Kielelezo 5.3b: Malipo wa Deni la Ndani

*Shilingi Bilioni*




*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu

### 5.1.5 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje inaendelea kuimarika, licha ya athari za mitikisiko ya uchumi duniani[6] . Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida (*current account deficit)* ilipungua kwa zaidi ya nusu hadi dola za Marekani milioni 1,908.2 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka uliopita (Jedwali 5.3). Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 15.8 hadi kufikia dola za Marekani milioni 12,314.7, sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilitokana na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii (Jedwali 5.4). Shughuli za utalii ziliimarika na kukua kwa asilimia 33.5 mwaka 2023, takribani sawa na kiwango kilichokuwepo kabla ya janga la UVIKO-19. Ukuaji huu unaakisi ongezeko la wastani wa matumizi kwa mtalii kwa siku na idadi ya watalii waliowasili nchini. Watalii waliendelea kutoka kwenye nchi ambazo huleta watalii wengi ikiwa ni pamoja na Marekani, Italia, Uingereza, Ufaransa na Ujerumani. Mauzo ya dhahabu yaliongezeka kwa asilimia 9.5 hadi dola za Marekani milioni 2,592.9, kutokana na kupanda kwa bei. Aidha, mauzo ya bidhaa asilia hususan, tumbaku, korosho na kahawa yaliongezeka zaidi ya matarajio, kwa asilimia 42.7 kufikia dola za Marekani milioni 1,001.3.

6 Mitikisiko ya uchumi duniani inahusisha migogoro ya kisiasa ya Mashariki ya Kati na mwendelezo wa hali ngumu ya kifedha katika uchumi wa nchi zilizoendelea, mabadiliko ya tabianchi pamoja utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kupunguza ukuaji wa ukwasi katika nchi zilizoendelea.

## Jedwali 5.3: Urari wa Malipo ya Kawaida

*Dola millioni*

| | Mwaka | | | Julai - Aprili | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023$^{p}$ | 2022/23 | 2023/24$^{p}$ |
| Urari wa bidhaa (halisi) | -3,247.1 | -6,984.9 | -6,032.3 | -6,099.9 | -4,981.8 |
| Zilizouzwa nje* | 6,756.2 | 7,223.8 | 7,696.6 | 6,092.3 | 6,583.7 |
| Zilizonunuliwa kutoka nje | -10,003.4 | -14,208.7 | -13,728.9 | -12,192.2 | -11,565.5 |
| Urari wa huduma (halisi) | 1,510.7 | 2,296.6 | 3,956.1 | 2,365.7 | 3,829.3 |
| Mapato | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,285.9 | 4,541.8 | 5,730.9 |
| Malipo | -1,607.0 | -2,465.4 | -2,329.8 | -2,176.1 | -1,901.7 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | -1,736.4 | -4,688.3 | -2,076.2 | -3,734.2 | -1,152.5 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 9,874.0 | 11,985.8 | 13,982.5 | 10,634.1 | 12,314.7 |
| Bishaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | -11,610.4 | -16,674.1 | -16,058.7 | -14,368.3 | -13,467.2 |
| Urari wa mapato ya vitega uchumi (halisi) | -1,191.6 | -1,393.2 | -1,505.7 | -1,164.9 | -1,254.6 |
| Yaliyoingia | 102.5 | 183.9 | 189.8 | 155.0 | 166.3 |
| Yaliyotoka | -1,294.2 | -1,577.1 | -1,695.5 | -1,319.9 | -1,420.9 |
| Urari wa uhamishaji Mali ya kawaida (halisi) | 553.7 | 599.3 | 646.0 | 492.0 | 498.9 |
| Iliyoingia | 640.1 | 716.5 | 791.9 | 587.5 | 646.9 |
| ambapo Serikalini | 104.7 | 76.4 | 111.8 | 40.9 | 74.3 |
| Iliyotoka | -86.4 | -117.2 | -145.9 | -95.6 | -147.9 |
| Urari wa bidhaa, huduma na uhamisho mapato (Halisi) | -2,374.3 | -5,482.2 | -2,935.9 | -4,407.2 | -1,908.2 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania

## Jedwali 5.4: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

*Dola milioni*

| | Mwaka | | | Julai - Aprili | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023$^{p}$ | 2022/23 | 2023/24$^{p}$ |
| Bidhaa asilia | 627.9 | 766.5 | 953.3 | 701.8 | 1,001.3 |
| Bidhaa zisizo asilia | 6,128.3 | 6,457.3 | 6,743.2 | 5,390.6 | 5,582.4 |
| ambapo dhahabu | 2,737.1 | 2,835.1 | 3,058.9 | 2,368.5 | 2,592.9 |
| Bidhaa za viwandani | 1,200.0 | 1,419.2 | 1,363.3 | 1,166.4 | 1,162.1 |
| Mazao ya mboga na maua | 378.6 | 289.6 | 417.2 | 262.0 | 379.2 |
| Mapato ya huduma | 3,117.7 | 4,762.0 | 6,285.9 | 4,541.8 | 5,730.9 |
| ambapo utalii | 1,310.3 | 2,527.8 | 3,373.8 | 2,472.1 | 3,102.5 |
| Usafirishaji | 1,558.1 | 1,872.0 | 2,426.0 | 1,713.4 | 2,173.8 |
| Mauzo ya bidhaa na huduma | 9,874.0 | 11,985.8 | 13,982.5 | 10,634.1 | 12,314.7 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania

Uagizaji wa bidhaa na huduma ulipungua kwa asilimia 6.3 hadi kufikia dola za Marekani milioni 13,467.2 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/23 (Jedwali 5.5). Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli, mitambo na vifaa vya viwandani, na mbolea. Uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli, ulipungua kwa asilimia 15.1 kufikia

dola za Marekani milioni 2,367.4 kutokana na kupungua kwa bei katika soko la dunia. Uagizaji wa mbolea ulishuka kwa asilimia 51.5 hadi dola za Marekani milioni 274.6, kutokana na kupungua kwa bei katika soko la dunia sambamba na kupungua kwa uagizaji wa mbolea kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mbolea nchini na akiba kutoka msimu uliopita. Kwa upande mwingine, ongezeko kubwa lilionekana kwenye uagizaji wa mashine na mitambo ya umeme, chuma na usafirishaji sambamba na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini.

### Jedwali 5.5: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

*Dola milioni*

| | Mwaka | | | Julai - April | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2021 | 2022 | 2023p | 2022/23 | 2023/24p |
| Bidhaa za kukuza mtaji | 1,710.6 | 2,594.0 | 2,893.4 | 2,418.3 | 2,362.2 |
| O/w Mashine na mitambo | 734.4 | 1,128.9 | 1,242.7 | 1,036.7 | 921.2 |
| Vifaa vya usafiri wa viwandani | 477.1 | 823.2 | 937.2 | 831.1 | 813.8 |
| Bidhaa za kati | 7,100.1 | 10,231.0 | 9,389.1 | 8,646.0 | 8,041.2 |
| Malighafi za viwanda | 3,375.7 | 4,780.1 | 4,307.1 | 3,902.2 | 3,702.2 |
| o/w Vyuma | 882.5 | 1,092.4 | 1,105.6 | 816.9 | 1,060.1 |
| Mbolea | 189.2 | 500.8 | 413.6 | 565.9 | 274.6 |
| Mafuta na vilainishi | 2,044.3 | 3,482.9 | 2,915.7 | 2,979.4 | 2,552.7 |
| o/w mafuta ya petroli | 1,942.5 | 3,314.8 | 2,725.8 | 2,787.5 | 2,367.4 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya viwandani | 586.1 | 717.9 | 828.8 | 690.3 | 721.7 |
| o/w Ngano | 204.9 | 302.4 | 418.8 | 313.7 | 281.9 |
| Mafuta ya kula yasiyosafishwa | 200.1 | 132.0 | 163.4 | 134.7 | 125.2 |
| Sukari | 109.6 | 135.6 | 125.4 | 118.1 | 122.5 |
| Bidhaa za kawaida | 1,190.4 | 1,381.5 | 1,444.2 | 1,126.1 | 1,160.3 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya kawaida | 167.5 | 182.0 | 240.1 | 193.9 | 147.6 |
| Bidhaa nyingine za kawaida | 908.9 | 1,040.1 | 1,062.4 | 804.9 | 885.6 |
| o/w Dawa na vifaa tiba | 333.8 | 342.9 | 307.0 | 249.2 | 239.8 |
| Nguo na vitambaa | 46.2 | 58.2 | 57.2 | 39.8 | 38.3 |
| Viatu na bidhaa zingine | 43.7 | 51.9 | 51.0 | 41.7 | 44.5 |
| Karatasi na bidhaa za karatasi | 24.3 | 26.8 | 26.7 | 21.6 | 26.6 |
| Jumla | 10,003.4 | 14,208.7 | 13,728.9 | 12,192.2 | 11,565.5 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

### 5.1.10 Mwenendo wa Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara na thabiti dhidi ya mitikisiko ya muda mfupi, huku viashiria vyote vya uimara wa sekta hii vikiwa ndani ya wigo unaokubalika. Katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024, sekta ya kibenki ilikuwa na ukwasi na mtaji wa kutosha na yenye

kutengeneza faida. Taasisi za kibenki zimeendelea kutumia teknolojia katika kutoa huduma za kifedha nchini, na hivyo kuongeza amana na rasilimali. Aidha, uwiano wa mtaji kwa rasilimali ulikuwa asilimia 19.4, juu ya ukomo unaokubalika kisheria wa asilimia 10. Ubora wa rasilimali uliendelea kuongezeka ambapo uwiano wa mikopo chechefu ulipungua hadi asilimia 4.3, Aprili 2024 kutoka asilimia 5.3, Juni 2023. Kupungua kwa mikopo chechefu kunatarajiwa kuchagiza ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi pamoja na kupungua kwa riba za mikopo.

Hata hivyo, Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua kadhaa kuhakikisha mikopo chechefu, inabaki ndani ya kiwango kinachokubalika. Hatua hizi ni pamoja na kusisitiza usimamizi unaozingatia udhibiti wa vihatarishi mbalimbali na kuzitaka benki kuboresha mchakato unaotumika katika kuidhinisha mikopo; kufuatilia taasisi za kibenki ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza mikakati waliyojiwekea katika kupunguza mikopo chechefu; na kuzitaka benki kuwasilisha taarifa za mikopo katika kanzi data ya taarifa za wakopaji. Vilevile, benki zimeendelea kuhimizwa kufuata Kanuni za Maadili za Jumuiya ya mabenki nchini, ili kuongeza uadilifu wa wafanyakazi.

### 5.1.11 Mifumo ya Malipo

Mifumo muhimu ya malipo (*Systemic Important Payment Systems*) iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi huku ikiendelea kuboreshwa ili kukidhi mahitaji. Benki Kuu imeweka ukomo wa tozo za miamala inayofanyika kupitia mfumo wa malipo makubwa (*TISS)* kuwa shilingi 10,000 na mfumo wa malipo madogo ya kidigitali (Electronic Fund Transfer (EFT)) kuwa shilingi 2000, ikiwa ni jitihada za kupunguza matumizi ya fedha taslimu katika kufanya miamala. Aidha, Benki Kuu imeendelea kutoa leseni kwa watoa huduma wasio taasisi za fedha (*merchant aggregators*) kwa kuwaidhinisha kutoa huduma za malipo ili

kupunguza matumizi ya fedha taslimu nchini. Ufuatiliaji wa mienendo ya mifumo ya malipo na watoa huduma za kifedha uliendelea kufanyika ili kuhakikisha usalama wa mifumo, na uadilifu wa watoa huduma wa mifumo hiyo.

Vilevile, Benki Kuu iliendelea kutekeleza mradi wa mfumo wa malipo madogo ya papo kwa papo (*Tanzania Instant Payment System-TIPS*) kwa kuongeza idadi ya washiriki. Mfumo huu ni miongoni mwa mipango ya Serikali katika kuondoa vikwazo na kupunguza gharama za kutuma fedha kati ya makundi mbalimbali ya watoa huduma za kifedha. Wakati huohuo, juhudi zimeendelea kufanyika ili kuunganisha mfumo huu na ule wa malipo ya serikali (GePG).


Katika kipindi kilichoishia mwezi April 2024, malipo madogo yaliyofanywa na taasisi za fedha kupitia mfumo wa EFT yaliongezeka huku miamala kupitia mfumo wa hundi ikipungua kwa kiasi kikubwa. Hali hii inaonesha kuwa, kwa sasa wananchi wengi wanapendelea mifumo ya kidijitali katika kufanya miamala kutokana na uhakika na usalama wake.

Idadi ya miamala ya hundi zilizo katika Shilingi ilipungua kwa asilimia 9.9, wakati hundi zilizo katika Dola za Marekani (USD) zilipungua kwa asilimia 27.3, huku thamani ya hundi husika zikipungua kwa asilimia 4.9 na 25.3, mtawalia (Kielelezo 5.4a na 5.4b). Kupungua kwa miamala ya hundi kunahusishwa na ongezeko la matumizi ya mifumo ya kielektroniki, benki mtandao, malipo kupitia simu, na mifumo ya malipo ya kikanda.

Simu za mkononi zimeendelea kuwa nyenzo muhimu ya kuwawezesha wananchi wasio na akaunti benki kupata huduma za kifedha. Thamani ya miamala ya malipo kupitia simu za mkononi iliongezeka kwa asilimia 35.2 kutokana na kupungua kwa tozo za miamala ya kawaida na ile ya kibiashara (*Merchants*) (Kielelezo 5.5b).

## Kielelezo 5.4a: Miamala ya Hundi za Shilingi


*Shilingi bilioni*




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania


## Kielelezo 5.4b: Miamala ya Hundi za Dola ya Marekani

*Dola milioni*





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 5.5a: Miamala Katika Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 5.5b Malipo Kupitia Simu




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania


## 5.2 Uchumi wa Zanzibar

### 5.2.1 Pato la Taifa

Mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2023 ulikuwa wa kuridhisha. Pato la taifa lilikua kwa asilimia 7.4 ikilinganishwa na asilimia 6.8 kwa mwaka 2022 (Kielelezo 5.6a). Ukuaji huu ulichangiwa na huduma za malazi na chakula hususan shughuli za utalii, ujenzi, ufugaji, upangishaji majengo na mazao (Kielelezo 5.6b).

**Kielelezo 5.6a: Ukuaji wa Pato la Taifa**


*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## Kielelezo 5.6b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Pato la Taifa

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

### 5.2.2 Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei ulikuwa tulivu, ukiwa juu kidogo ya lengo la muda wa kati la asilimia 5. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Aprili 2024, mfumuko wa bei ulikuwa ni wastani wa asilimia 5.9, ukipungua toka wastani wa asilimia 7.1 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula. Mfumuko wa bei za vyakula ulikuwa asilimia 10.3, ukiwa ni juu kidogo ya asilimia 10 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za vyakula, ulikuwa ni wastani wa asilimia 2.9, ukiwa chini ya asilimia 5 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita, kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa katika soko la dunia (Kielelezo 5.7).

**Kielelezo 5.7: Mfumuko wa Bei**




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

### 5.2.3 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali


Mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yakijumuisha mapato ya ndani na misaada toka nje, yaliongezeka kufikia shillingi billioni 1,353.1 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Aprili 2023/24, ikiwa ni juu ya lengo kwa asilimia 5. Kati ya mapato yote yaliyokusanywa, mapato ya ndani yalikuwa shillingi bilioni 1,238.5, sawa na asimilia 99.7 ya lengo, wakati misaada ilikuwa ni shilingi bilioni 114.6. Mapato ya kodi, yalikuwa shillingi bilioni 1,095.1, juu ya lengo kwa asilimia 2.9. Mwenendo huu ulitokana na kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji kodi na ufuatiliaji, na mwamko wa wananchi kulipa kodi kwa hiari. Wakati huo huo, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 143.3, sawa na asilimia 80.3 ya lengo (Kielelezo 5.8a).

Matumizi ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,693.9, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 986.7 na kiasi kilichobakia kilitumika kugharamia shughuli za maendeleo (Kielelezo 5.8b). Mapato toka vyanzo vya ndani yaliyotumika kugharamia miradi ya maendeleo

yalikuwa shilingi bilioni 571.4, wakati toka vyanzo vya nje yalikuwa shilingi bilioni 135.9. Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada ilikuwa shilingi bilioni 455.5, ikigharamiwa na mikopo toka ndani na nje ya nchi.

**Kielelezo 5.8a: Mapato ya Serikali**


*Shilingi billioni*




*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

**Kielelezo 5.8b: Matumizi ya Serikali**

*Shilingi bilioni*





*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

### 5.2.4 Deni la Serikali

Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilifikia shilingi bilioni 3,567.9 mwezi Aprili 2024, ukilinganisha na shilingi bilioni 2,737.9 mwezi Juni 2023, ambapo deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 2,638.2 (sawa na dola za Marekani milioni 1,025.5) ukilinganisha na shilingi bilioni 2,396.5 mwezi Juni 2023. Kuongezeka kwa deni kulitokana na mikopo mipya na kushuka kwa thamani ya shilingi. Deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 929.6, ikiwa ni ongezeko toka shilingi bilioni 341.4 kwa mwezi Juni 2023, kutokana na mikopo mipya kupitia hatifungani za Serikali na ukopaji kutoka taasisi za umma (Kielelezo 5.9).

#### Kielelezo 5.9: Mwenendo wa Deni la Serikali

*Shilingi bilioni*




*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

### 5.2.5 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Urari wa malipo ya kawaida uliimarika hadi kufikia ziada ya dola za Marekani milioni 484.6 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, ukilinganisha na ziada ya dola za Marekani milioni 396.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23 (Jedwali Na 5.6). Ongezeko hili lilitokana

na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kwa asilimia 9.9 hadi dola za Marekani milioni 976.3, kutokana na kuimarika kwa sekta ya utalii (Kielelezo 5.10a). Mapato ya huduma hasa utalii yalikuwa takribani asilimia 94 ya mapato yote ya huduma na bidhaa toka nje. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka kwa asilimia 0.5 hadi dola za Marekani milioni 503.8, kutokana na kuongezeka kwa uagizaji wa vifaa vya usafirishaji, ujenzi na bidhaa za vyakula (Kielelezo 5.10b).

## Jedwali 5.6: Zanzibar: Urari wa Malipo ya Kawaida


*Dola milioni*

| | Mwaka unaoshia Aprili | | | Jul- Apr | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024p | 2023 | 2024p |
| Urari wa bidhaa (halisi) | -279.2 | -425.7 | -414.9 | -358.6 | -361.0 |
| Zilizouzwa nje | 87.4 | 64.8 | 87.4 | 61.5 | 61.3 |
| Zilizonunuliwa kutoka nje | 366.6 | 490.5 | 502.2 | 420.2 | 422.4 |
| Urari wa huduma (halisi) | 560.1 | 817.3 | 923.3 | 745.9 | 833.5 |
| Mapato | 631.9 | 910.9 | 1,020.3 | 827.0 | 914.9 |
| Malipo | 71.8 | 93.6 | 97.0 | 81.0 | 81.4 |
| Urari wa bidhaa na huduma (halisi) | 280.9 | 391.6 | 508.4 | 387.3 | 472.5 |
| Bidhaa na huduma zilizouzwa nje | 719.4 | 975.7 | 1,107.7 | 888.5 | 976.3 |
| Bishaa na huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 438.4 | 584.1 | 599.2 | 501.2 | 503.8 |
| Urari wa mapato ya msingi (halisi) | 3.5 | 7.5 | 12.1 | 8.1 | 10.6 |
| Yaliyoingia | 6.7 | 11.1 | 17.7 | 11.0 | 15.5 |
| Yaliyotoka | 3.2 | 3.6 | 5.6 | 2.9 | 4.9 |
| Urari wa Uhamishaji Mali (halisi) | 10.2 | 1.1 | 1.7 | 0.9 | 1.5 |
| Iliyoingia | 14.9 | 1.9 | 3.0 | 1.5 | 2.6 |
| Iliyotoka | 4.7 | 0.8 | 1.2 | 0.6 | 1.1 |
| Urari wa Bidhaa, huduma na uhamishaji mali | 294.6 | 400.2 | 522.2 | 396.3 | 484.6 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania
*Ufafanuzi:* p inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 5.10a: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi


*Dola millioni*




*Chanzo:*Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 5.10b: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nje

*Dola millioni*




*Chanzo:*Mamlaka ya Mapato na Benki Kuu ya Tanzania

# SEHEMU YA SITA

## 6.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI

### 6.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia.

Ukuaji wa uchumi wa dunia unatarajiwa kuendelea kuimarika. Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili 2024, inakadiria uchumi wa dunia kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2024 na 2025, ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.1 ukilinganisha na makadirio ya Januari 2024. Makadirio haya yanatokana na matarajio ya benki kuu za nchi zilizoendelea kuanza kupunguza riba za sera ya fedha sambamba na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka katika nchi zilizoendelea, zile zinaibuka kiuchumi pamoja na nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara[5]. Matarajio haya yanatokana na kupungua kwa athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi pamoja na kuimarika kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa duniani. Aidha, matarajio hayo yatategemea mabadiliko ya bei za nishati, migogoro ya kisiasa na maamuzi ya benki kuu za nchi zilizoendelea kuhusu mwelekeo wa riba katika kutekeleza sera ya fedha. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha, na kutengemaa kwa mnyororo wa ugavi wa bidhaa duniani. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua kutokana na hatua za kisera zinazochukuliwa na nchi wanachama na upatikanaji wa chakula. Mwenendo huu wa mfumuko wa bei utategemea maamuzi ya umoja wa nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi duniani (OPEC+) kuhusu kiwango cha uzalishaji na migogoro ya kisiasa duniani.


5 Ukuaji katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 3.8 kwa mwaka 2024 na asilimia 4 kwa mwaka 2025.

## 6.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani

Uchumi wa Tanzania, unatarajiwa kuendelea kuimarika, sambamba na kutengemaa kwa mazingira ya kiuchumii duniani na ndani ya nchi. Uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 5.8 mwaka 2025, ukichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini. Ukuaji katika sekta ya kilimo utachagizwa na matarajio ya kuwepo kwa mvua za kutosha nchini pamoja na utekelezaji wa sera mbalimbali zinazolenga kuchochea uzalishaji katika sekta ya kilimo na mnyororo mzima wa uzalishaji katika sekta hii. Ukuaji katika shughuli za ujenzi unategemea uwekezaji unaondelea kufanyika katika miundombinu, wakati kuimarika kwa sekta ya madini kunategemea ongezeko la uzalishaji katika migodi iliyopo na uwekezaji mpya katika uchimbaji wa madini. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2024 na 6.8 mwaka 2025, ukichangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na viwanda. Matarajio ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar yanaakisi matarajio ya kukamilika kwa miradi mikubwa ya ujenzi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la asilimia 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, uhakika wa upatikanaji wa umeme na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

## Kielelezo 6.1a: Ukuaji na Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi kwa Tanzania Bara


*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar na Uchambuzi wa Benki Kuu

## Kielelezo 6.1b: Ukuaji na Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi kwa Zanzibar

*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar na Uchambuzi wa Benki Kuu

Urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuendelea kuimarika, hadi kufikia wastani wa asilimia 3.2 ya Pato la Taifa, katika kipindi cha muda wa kati, sawia na kiwango kilichofikiwa kabla ya Janga la UVIKO-19. Urari huu unatarajiwa kuimarika mwaka 2024/25, ukichangiwa na matarajio ya ongezeko la mauzo ya dhahabu nje ya nchi kutokana na bei nzuri katika soko la dunia, pamoja na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya kilimo kutokana na mvua za kutosha na mikakati ya serikali ya kuboresha uzalishaji na masoko. Aidha, mapato ya utalii yanatarajiwa kuendelea kuongezeka. Vilevile, uagizaji wa bidhaa kutoka nje unatarajiwa kuongezeka kwa kiasi, sambamba na hatua zinazoendelea kuchukuliwa ili kuongeza mauzo nje ya nchi na kupunguza uagizaji kutoka nje ya nchi. Vihatarishi vya kutofikiwa kwa matarajio hayo ni pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta kutokana na nchi wanachama wa OPEC+ kupunguza uzalishaji wa mafuta na kuendelea kwa migogoro ya kisiasa inayoweza kusababisha ongezeko la bei za mafuta katika soko la dunia.

# SEHEMU YA SABA

## 7.0 SERA YA FEDHA YA MWAKA 2024/25

### 7.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha

Katika mwaka 2024/25, sera ya fedha inalenga kuendelea kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 na kuwezesha ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 mwaka 2024 na asilimia 5.8 mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na asilimia 7.2 na asilimia 6.8 kwa Zanzibar. Mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 ni kupunguza kasi ya ongezeko la ukwasi ili kukabiliana na athari zinazotokana na kushuka kwa thamani ya shilingi kwenye mfumuko wa bei. Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR), ambayo itafanyiwa mapitio kila robo mwaka. Aidha Benki Kuu itaendelea kutumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha riba ya mikopo ya siku 7 baina ya mabenki inabaki ndani ya wigo wa riba ya Benki Kuu. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuelimisha umma kuhusu mfumo mpya wa sera ya fedha, kutoa taarifa na maamuzi ya kamati ya sera ya fedha na kuchapisha kalenda ya mikutano ya kamati ya Sera ya Fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha, yakilenga kuongeza ufanisi katika usambazaji wa ukwasi pamoja na kuongeza uthabiti na ujumuishi wa sekta ya fedha. Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza ufanisi wa sera ya fedha ili kuweza kufikia malengo yake ya kudhibiti mfumuko wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi.

## 7.2 Sera ya Riba

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa na nguvu za soko. Mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, utaendelea kuchangia katika kuwezesha taasisi za fedha kupanga riba kwa kuzingatia nguvu ya soko. Hivyo basi, riba ya Benki Kuu (CBR), itatumika kama kigezo kimojawapo katika ukokotoaji wa viwango vya riba. Hii itaenda sambamba na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika kutekeleza maboresho katika sekta ya fedha, kuboresha jitihada za kumlinda mlaji, kutoa elimu ya fedha na huduma jumuishi za kifedha.

## 7.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni

Viwango vya ubadilishaji fedha za kigeni vitaendelea kuamuliwa na nguvu za soko, ikiwa ni njia ya msingi ya kuzuia madhara ya mitikisiko ya uchumi toka nje ya nchi. Benki Kuu itaendelea kufuatilia na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya mabenki (IFEM) kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki ya Soko la Fedha za Kigeni (Foreign Exchange Intervention Policy) na kuhakikisha washiriki wanafuata kanuni za maadili ya IFEM (IFEM code of conduct). Aidha, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni ili iweze kutumika kama kinga dhidi ya mitikisiko kutoka nje ya nchi. Vilevile, kupungua kwa riba za sera za fedha katika nchi zilizoendelea, kunatarajiwa kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni nchini, hususan dola za Marekani, na hivyo kupunguza shinikizo kwenye akiba ya fedha za kigeni na viwango vya ubadilishaji fedha.

# VIAMBATISHO

## Jedwali 1: Tanzania Bara: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

*Asilimia*

| Shughuli za kiuchumi | 2018 | 2019 | 2020r | 2021r | 2022r | 2023p |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 5.4 | 4.4 | 4.9 | 3.9 | 3.3 | 4.2 |
| Kilimo cha mazao | 5.2 | 4.4 | 5.0 | 3.6 | 2.7 | 4.2 |
| Mifugo | 4.9 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 4.9 | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 |
| Uvuvi | 9.2 | 1.5 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 |
| Viwanda na ujenzi | 9.7 | 11.4 | 6.7 | 4.9 | 5.3 | 5.1 |
| Uchimbaji madini na mawe | 1.5 | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 |
| Viwanda | 8.3 | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 |
| Umeme | 5.8 | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 |
| Maji safi na maji taka | 7.4 | 6.9 | 5.8 | 6.5 | 5.5 | 2.5 |
| Ujenzi | 13.7 | 13.3 | 7.8 | 3.3 | 3.9 | 3.5 |
| Huduma | 6.5 | 5.9 | 4.3 | 4.8 | 5.3 | 5.8 |
| Biashara na matengenezo | 6.6 | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 11.8 | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 |
| Malazi na huduma ya chakula | 5.2 | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 |
| Habari na mawasiliano | 9.1 | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 |
| Fedha na bima | -0.5 | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 12.2 |
| Upangishaji majengo | 4.4 | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | 9.9 | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 5.6 | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 |
| Utawala na ulinzi | 3.2 | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 |
| Elimu | 6.6 | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 |
| Afya na huduma za jamii | 8.4 | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 |
| Sanaa na burudani | 13.7 | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 |
| Huduma nyingine za kijamii | 6.5 | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 |
| Shughuli za kaya katika kuajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 |
| Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM) | 7.1 | 7.1 | 5.2 | 4.6 | 4.8 | 5.2 |
| Kodi za bidhaa | 6.3 | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 7.0 | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 |

*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali 2: Zanzibar: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi

*Asilimia*

| Shughuli za kiuchumi | 2018 | 2019 | 2020[r] | 2021[r] | 2022[p] | 2023[p] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 3.7 | 2.6 | 3.3 | 2.6 | 4.0 | 2.3 |
| Kilimo cha mazao | 3.7 | -5.8 | 1.3 | 2.2 | 6.1 | 2.8 |
| Mifugo | 7.7 | 17.0 | 8.2 | 3.0 | 2.3 | -4.3 |
| Misitu | 0.3 | 3.8 | -4.4 | 4.0 | 2.9 | 6.4 |
| Uvuvi | 1.0 | 3.3 | 3.5 | 2.3 | 3.0 | 8.1 |
| Viwanda na ujenzi | 3.8 | 10.6 | 5.2 | 5.1 | 9.3 | 6.6 |
| Uchimbaji madini na mawe | 13.3 | -1.7 | -6.0 | 9.9 | 9.1 | 10.4 |
| Viwanda | 2.1 | 20.5 | 6.5 | 1.1 | 8.1 | 6.9 |
| Umeme | 5.1 | 5.2 | -3.2 | 8.0 | 22.3 | 12.4 |
| Maji safi na maji taka | 2.8 | 12.9 | 2.0 | 6.9 | 7.0 | 4.6 |
| Ujenzi | 4.1 | 3.1 | 6.5 | 8.9 | 10.2 | 5.5 |
| Huduma | 10.2 | 8.6 | 7.4 | 6.9 | 7.7 | 9.9 |
| Biashara na matengenezo | 8.0 | 9.1 | 1.0 | 14.9 | 4.2 | 12.6 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 9.4 | 4.7 | -6.6 | 9.3 | 3.8 | 9.2 |
| Malazi na huduma ya chakula | 17.6 | 11.5 | -12.7 | 6.6 | 11.7 | 8.2 |
| Malazi | 17.0 | 11.8 | -11.3 | 6.5 | 12.3 | 7.8 |
| Chakula na vinywaji | 20.3 | 10.0 | -18.9 | 7.5 | 9.0 | 9.8 |
| Habari na mawasiliano | 3.4 | 5.5 | -3.2 | -16.3 | 2.5 | -10.8 |
| Fedha na bima | 4.4 | 3.1 | 2.2 | 9.9 | 3.7 | 54.6 |
| Upangishaji majengo | 6.4 | 6.6 | 6.8 | 7.0 | 7.1 | 7.2 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | 5.2 | -2.9 | 1.1 | 5.0 | 1.4 | 3.5 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 4.9 | 6.9 | -4.6 | 6.6 | -1.5 | 17.0 |
| Utawala na ulinzi | 5.5 | 11.7 | 13.2 | 5.3 | 8.2 | 2.1 |
| Elimu | 7.0 | 7.5 | 9.7 | -0.3 | 9.8 | 3.7 |
| Afya na huduma za jamii | 2.3 | 2.5 | 1.4 | 2.4 | 8.9 | 15.8 |
| Sanaa na burudani | 19.3 | 3.3 | -4.9 | 1.1 | 1.9 | 33.8 |
| Huduma nyingine za kijamii | 14.2 | 2.0 | 12.9 | 6.9 | 6.2 | 8.8 |
| Shughuli za kaya katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 2.9 | 2.6 |
| Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM) | -10.2 | 2.6 | 11.7 | 2.8 | 6.5 | 38.1 |
| Kodi za bidhaa | 3.8 | 1.6 | 1.6 | 1.2 | 3.0 | 5.9 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 7.1 | 7.0 | 1.3 | 5.1 | 6.8 | 7.4 |

*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar*

# Jedwali 3: Tanzania Bara: Mfumuko wa Bei

*Asilimia*

| Bidhaa na Huduma | Mizania (%) | Apr-23 | May-23 | Jun-23 | Jul-23 | Aug-23 | Sep-23 | Oct-23 | Nov-23 | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vyakula na vinywaji baridi | 28.2 | 9.1 | 8.5 | 7.8 | 6.1 | 5.6 | 5.6 | 4.5 | 3.7 | 2.3 | 1.5 | 1.8 | 1.4 | 1.4 |
| Vinywaji vikali na tumbaku | 1.9 | 0.8 | 1.5 | 1.7 | 3.8 | 3.7 | 3.6 | 3.5 | 4.1 | 4.1 | 4.1 | 4.2 | 4.3 | 4.0 |
| Mavazi na viatu | 10.8 | 2.8 | 3.3 | 3.5 | 3.4 | 3.4 | 3.0 | 3.0 | 3.3 | 3.2 | 2.8 | 2.7 | 2.4 | 2.1 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 15.1 | 0.3 | 0.8 | 1.1 | 1.2 | 1.4 | 1.3 | 1.0 | 2.8 | 4.0 | 4.9 | 5.0 | 4.8 | 5.2 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 7.9 | 3.1 | 2.9 | 2.5 | 2.7 | 4.1 | 3.9 | 3.4 | 3.6 | 3.6 | 3.3 | 3.5 | 3.6 | 3.3 |
| Afya | 2.5 | 1.8 | 1.7 | 1.3 | 1.9 | 2.1 | 1.7 | 1.7 | 1.4 | 1.3 | 1.8 | 2.1 | 2.1 | 2.0 |
| Usafiri | 14.1 | 4.3 | 1.3 | -0.4 | 0.4 | 0.6 | 1.0 | 3.1 | 2.9 | 3.3 | 3.3 | 2.9 | 4.4 | 5.1 |
| Habari na mawasiliano | 5.4 | 1.7 | 1.8 | 1.9 | 2.1 | 2.1 | 1.7 | 1.4 | 1.3 | 1.3 | 1.0 | 1.9 | 1.9 | 1.8 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.6 | 1.8 | 1.9 | 1.9 | 2.2 | 2.5 | 2.7 | 2.8 | 3.4 | 3.5 | 3.8 | 3.6 | 3.4 | 3.3 |
| Huduma za elimu | 2.0 | 3.3 | 3.7 | 3.3 | 3.3 | 3.3 | 3.5 | 3.5 | 3.5 | 3.5 | 2.7 | 2.8 | 2.8 | 2.8 |
| Migahawa na huduma za malazi | 6.6 | 3.2 | 4.8 | 5.1 | 5.1 | 5.1 | 5.4 | 4.9 | 4.5 | 4.3 | 5.0 | 4.6 | 4.1 | 4.1 |
| Huduma za bima na fedha | 2.1 | -0.4 | -0.4 | -0.4 | 0.2 | 0.2 | 0.1 | 0.6 | 0.6 | 0.6 | 0.7 | 1.0 | 1.6 | 1.5 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko | 2.1 | 1.6 | 1.7 | 2.6 | 3.9 | 4.0 | 3.9 | 3.6 | 3.5 | 4.5 | 7.1 | 7.1 | 7.3 | 7.5 |
| Fahirisi bidhaa zote | 100.0 | 4.3 | 4.0 | 3.6 | 3.3 | 3.3 | 3.3 | 3.2 | 3.2 | 3.0 | 3.0 | 3.0 | 3.0 | 3.1 |
| Makundi mengine maalumu | | | | | | | | | | | | | | |
| Mfumuko wa bei wa msingi | 73.9 | 2.0 | 2.0 | 1.7 | 2.1 | 2.2 | 2.3 | 2.5 | 2.6 | 3.1 | 3.2 | 3.7 | 3.9 | 3.9 |
| Mfumuko wa bei usio wa msingi | 26.1 | 10.7 | 9.4 | 8.7 | 6.6 | 6.4 | 6.3 | 5.0 | 5.0 | 3.2 | 2.2 | 1.4 | 0.9 | 1.4 |
| Nishati, mafuta na ankara za maji | 5.7 | 0.4 | -1.1 | | | | 0.9 | 0.8 | 5.3 | 5.1 | 6.6 | 7.2 | 6.6 | 9.3 |
| Huduma | 37.2 | 2.6 | 2.2 | 1.6 | 2.1 | 2.2 | 2.2 | 2.7 | 2.6 | 3.2 | 3.4 | 3.0 | 3.3 | 3.3 |
| Bidhaa | 62.8 | 5.3 | 5.0 | 4.7 | 4.0 | 4.0 | 4.0 | 3.4 | 3.7 | 3.1 | 2.7 | 3.0 | 2.8 | 3.1 |
| Huduma za elimu na bidhaa zinazohusiana na elimu | 4.1 | 2.0 | 2.3 | 2.3 | 3.0 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.2 | 3.6 | 3.0 | 2.9 | 3.0 | 3.1 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zote isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 71.8 | 2.3 | 2.1 | 1.8 | 2.2 | 2.4 | 2.4 | 2.6 | 3.0 | 3.3 | 2.8 | 3.5 | 3.7 | 3.9 |

*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali 4: Zanzibar: Mfumuko wa Bei

*Asilimia*

| Bidhaa na huduma | Mizania (%) | Apr-23 | May-23 | Jun-23 | Jul-23 | Aug-23 | Sep-23 | Oct-23 | Nov-23 | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei wa jumla | 100.0 | 7.5 | 6.4 | 6.5 | 6.7 | 6.8 | 7.5 | 6.5 | 6.3 | 5.5 | 5.3 | 5.1 | 4.9 | 4.9 |
| Mfumuko wa bei wa chakula | 41.9 | 11.5 | 9.5 | 10.7 | 11.8 | 12.0 | 14.4 | 11.6 | 10.9 | 8.8 | 9.2 | 8.9 | 7.6 | 8.0 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula | 58.6 | 4.8 | 4.3 | 3.6 | 3.2 | 3.2 | 2.7 | 3.0 | 3.0 | 3.2 | 2.5 | 2.4 | 3.0 | 2.6 |
| Minywaji vikali na tumbaku | 0.2 | 0.0 | 0.0 | 0.7 | 0.7 | 11.7 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | -3.1 | 4.8 | 23.8 | 23.8 | 23.8 |
| Mavazi na viatu | 6.3 | 3.7 | 3.5 | 3.0 | 3.1 | 0.7 | 2.4 | 2.6 | 2.4 | 3.1 | 0.0 | 3.3 | 3.6 | 1.3 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 25.8 | 3.7 | 3.7 | 2.4 | 1.4 | 3.2 | 1.2 | 1.8 | 1.8 | 1.4 | 2.5 | 1.4 | 2.3 | 2.1 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 4.8 | 6.7 | 6.1 | 7.1 | 7.5 | 1.7 | 7.3 | 6.3 | 5.5 | 9.0 | 3.0 | 3.1 | 3.4 | 2.9 |
| Afya | 1.3 | 12.3 | 13.1 | 10.4 | 10.3 | 8.2 | 9.6 | 7.5 | 7.0 | 5.9 | 9.5 | 0.4 | -1.2 | -1.5 |
| Usafiri | 9.1 | 11.5 | 9.3 | 7.0 | 5.5 | 10.5 | 5.5 | 6.6 | 7.5 | 3.4 | 2.5 | 2.6 | 3.5 | 4.0 |
| Habari na mawasiliano | 4.2 | 1.1 | 1.1 | 1.1 | 1.0 | 5.5 | 0.7 | 0.7 | 0.7 | 1.6 | 11.2 | 0.8 | 1.1 | 1.4 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.1 | 0.3 | -1.3 | -1.3 | -0.8 | 1.0 | 7.1 | 7.3 | 7.2 | 0.1 | 1.7 | 8.5 | 8.6 | 4.4 |
| Huduma za elimu | 1.6 | 3.4 | 3.4 | 3.4 | 14.5 | 7.1 | 3.7 | 5.1 | 5.1 | 8.3 | 3.8 | 2.1 | 2.1 | 2.3 |
| Migahawa na huduma za malazi | 1.4 | 1.7 | 1.9 | 1.2 | 1.3 | 3.7 | -2.3 | -3.0 | -3.0 | -0.5 | 0.0 | 11.3 | 11.3 | 11.3 |
| Huduma za bima na fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko | 1.7 | 3.8 | 3.7 | 2.2 | 2.2 | 2.3 | 1.9 | 2.7 | 2.7 | 2.5 | 3.6 | 4.7 | 5.3 | 2.9 |

*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar*

# Jedwali 5: Takwimu za Kifedha

*Shilingi billioni*

| | Apr-23 | May-23 | Jun-23 | Jul-23 | Aug-23 | Sep-23 | Oct-23 | Nov-23 | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 8,635.9 | 7,811.0 | 10,455.1 | 10,769.2 | 10,934.9 | 10,121.6 | 9,380.5 | 9,970.8 | 11,302.4 | 10,376.1 | 10,242.9 | 11,635.0 | 10,091.9 |
| Rasilimali halisi za Benki Kuu | 10,000.6 | 9,513.8 | 11,333.3 | 11,384.6 | 11,288.4 | 10,646.8 | 9,986.2 | 10,644.3 | 12,079.3 | 11,263.9 | 11,025.8 | 11,981.8 | 10,896.0 |
| *Akiba halisi ya fedha za kigeni (Dola milioni)* | *4,881.2* | *4,695.9* | *5,446.1* | *5,338.9* | *5,208.3* | *4,880.4* | *4,615.0* | *4,850.6* | *5,450.1* | *5,107.1* | *4,971.5* | *5,327.1* | *4,885.8* |
| Rasilimali halisi za mabenki | -1,364.7 | -1,702.9 | -878.2 | -615.4 | -353.5 | -525.2 | -605.7 | -673.5 | -776.9 | -887.8 | -782.9 | -346.8 | -804.1 |
| *Rasilimali halisi za mabenki (Dola milioni)* | *-589.9* | *-734.2* | *-377.1* | *-256.2* | *-144.6* | *-211.6* | *-244.0* | *-269.3* | *-310.6* | *-352.8* | *-307.7* | *-135.5* | *-312.5* |
| Rasilimali halisi katika shilingi ya Tanzania | 31,325.6 | 32,368.6 | 31,729.8 | 31,872.6 | 32,203.2 | 33,019.5 | 33,575.4 | 33,614.1 | 32,700.2 | 33,381.3 | 33,726.5 | 32,892.0 | 34,226.6 |
| Madai ya ndani | 40,193.8 | 40,893.6 | 41,586.2 | 41,468.8 | 41,885.0 | 42,586.6 | 43,884.1 | 44,539.0 | 43,411.5 | 44,384.1 | 44,991.7 | 44,217.1 | 44,916.3 |
| Madai halisi kwa Serikali Kuu | 11,490.9 | 11,732.5 | 11,750.6 | 11,408.8 | 11,276.2 | 11,795.4 | 12,667.7 | 12,666.4 | 11,353.9 | 12,003.5 | 12,331.0 | 10,876.6 | 11,169.8 |
| Madai kwa Serikali Kuu | 20,141.7 | 21,585.1 | 19,213.5 | 19,424.7 | 20,048.7 | 21,276.8 | 22,443.1 | 22,889.7 | 22,799.1 | 23,125.4 | 23,440.9 | 22,328.7 | 23,125.5 |
| Dhamana za Serikali | 8,681.4 | 8,789.6 | 8,853.5 | 8,980.5 | 8,988.0 | 9,026.2 | 8,979.3 | 8,651.5 | 8,641.5 | 8,412.8 | 8,681.6 | 8,513.8 | 8,167.2 |
| Amana za Serikali | 8,650.8 | 9,852.6 | 7,462.9 | 8,015.9 | 8,772.6 | 9,481.4 | 9,775.4 | 10,223.3 | 11,445.2 | 11,121.9 | 11,110.0 | 11,452.1 | 11,955.8 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 28,702.9 | 29,161.2 | 29,835.6 | 30,060.0 | 30,608.8 | 30,791.3 | 31,216.4 | 31,872.6 | 32,057.6 | 32,380.6 | 32,660.7 | 33,340.5 | 33,746.5 |
| Mikopo iliyotolewa kwa shilingi ya Tanzania | 20,531.0 | 21,018.8 | 21,684.6 | 22,278.2 | 22,918.0 | 23,117.9 | 23,504.6 | 23,761.3 | 24,154.1 | 24,428.4 | 24,726.5 | 25,047.0 | 25,729.0 |
| Mikopo iliyotolewa kwa fedha za kigeni | 8,171.9 | 8,142.4 | 8,150.9 | 7,781.8 | 7,690.8 | 7,673.4 | 7,711.8 | 8,111.3 | 7,903.5 | 7,952.2 | 7,934.2 | 8,293.5 | 8,017.5 |
| Mikopo (Kwenye Dola milioni za Marekani) | *3,533.6* | *3,515.0* | *3,508.8* | *3,330.4* | *3,164.9* | *3,112.1* | *3,106.3* | *3,255.7* | *3,164.7* | *3,169.3* | *3,139.1* | *3,257.4* | *3,117.3* |
| Rasilimali nyinginezo (Other Items Net) | -8,868.2 | -8,525.0 | -9,856.3 | -9,596.2 | -9,681.8 | -9,567.2 | -10,308.7 | -10,924.9 | -10,711.3 | -11,002.8 | -11,265.2 | -11,325.1 | -10,689.7 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3 | 39,961.5 | 40,179.6 | 42,185.0 | 42,641.8 | 43,138.1 | 43,141.0 | 42,955.9 | 43,584.9 | 44,002.6 | 43,757.4 | 43,969.4 | 44,527.0 | 44,318.4 |
| Amana za fedha za kigeni (FCD) | 8,912.7 | 8,836.9 | 9,591.3 | 9,830.1 | 9,851.5 | 9,715.9 | 9,496.3 | 10,148.5 | 10,000.8 | 9,990.5 | 10,132.6 | 10,397.3 | 10,493.7 |
| Amana za fedha za kigeni (Dola milioni) | *3,854.0* | *3,814.8* | *4,128.8* | *4,207.0* | *4,054.1* | *3,940.5* | *3,825.1* | *4,073.4* | *4,004.6* | *3,981.7* | *4,009.0* | *4,083.6* | *4,080.0* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 31,048.8 | 31,342.7 | 32,593.7 | 32,811.7 | 33,286.6 | 33,425.2 | 33,459.6 | 33,436.4 | 34,001.7 | 33,766.9 | 33,836.7 | 34,129.6 | 33,824.8 |
| Amana nyinginezo | 11,800.6 | 12,056.4 | 12,241.3 | 12,306.6 | 12,514.7 | 12,813.9 | 12,891.0 | 13,149.6 | 13,400.1 | 13,272.7 | 13,290.2 | 13,266.6 | 13,561.2 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 19,248.3 | 19,286.2 | 20,352.4 | 20,505.1 | 20,771.9 | 20,611.2 | 20,568.6 | 20,286.8 | 20,601.6 | 20,494.2 | 20,546.6 | 20,863.0 | 20,263.6 |
| Fedha zilizopo kwenye mzunguko | 5,424.8 | 5,646.0 | 6,161.5 | 6,347.7 | 6,460.7 | 6,475.9 | 6,316.8 | 6,373.1 | 6,486.4 | 6,108.1 | 6,083.9 | 6,325.7 | 6,147.0 |
| Amana za hundi | 13,823.5 | 13,640.2 | 14,190.9 | 14,157.4 | 14,311.2 | 14,135.3 | 14,251.8 | 13,913.7 | 14,115.2 | 14,386.1 | 14,462.7 | 14,537.3 | 14,116.6 |
| Memorandum Items | | | | | | | | | | | | | |
| Fedha Taslimu | 9,463.3 | 9,590.1 | 10,850.7 | 10,194.8 | 10,392.8 | 9,943.7 | 9,825.2 | 10,066.5 | 10,099.8 | 10,411.9 | 10,138.1 | 10,185.5 | 10,066.6 |
| Akiba za benki | 3,028.0 | 2,945.4 | 3,658.6 | 2,746.0 | 2,877.8 | 2,411.2 | 2,413.1 | 2,644.3 | 2,444.5 | 3,221.1 | 3,036.4 | 2,907.0 | 2,835.7 |
| Fedha zilizo nje ya Benki Kuu ya Tanzania | 6,435.3 | 6,644.7 | 7,192.0 | 7,448.8 | 7,515.1 | 7,532.5 | 7,412.1 | 7,422.2 | 7,655.3 | 7,190.8 | 7,101.7 | 7,278.5 | 7,230.9 |
| Wastani wa Fedha Taslimu | 9,408.4 | 9,666.5 | 9,797.4 | 10,203.2 | 10,356.9 | 10,387.8 | 10,162.1 | 9,965.8 | 10,183.6 | 10,261.1 | 10,401.5 | 10,534.6 | 10,305.9 |
| Kiwango cha ubadilishaji fedha (mwisho wa kipindi) | 2,312.6 | 2,316.5 | 2,323.0 | 2,336.6 | 2,430.0 | 2,465.6 | 2,482.6 | 2,491.4 | 2,497.4 | 2,509.1 | 2,527.5 | 2,546.1 | 2,572.0 |
| Akiba ya fedha za kigeni (Dola milioni) | 4,881.2 | 4,695.9 | 5,446.1 | 5,338.9 | 5,208.3 | 4,880.4 | 4,615.0 | 4,850.6 | 5,450.1 | 5,107.1 | 4,971.5 | 5,327.1 | 4,885.8 |
| Rasilimali za nje za benki (Dola milioni) | 1,088.9 | 1,221.5 | 1,333.3 | 1,623.3 | 1,713.9 | 1,795.8 | 1,680.1 | 1,628.5 | 1,662.3 | 1,623.5 | 1,672.8 | 1,745.9 | 1,389.2 |
| Jumla ya Rasilimali za nje katika benki (Dola milioni) | 5,970.1 | 5,917.4 | 6,779.3 | 6,962.2 | 6,922.2 | 6,676.1 | 6,295.1 | 6,479.1 | 7,112.4 | 6,730.6 | 6,644.4 | 7,073.1 | 6,275.0 |
| Viwango vya ukuaji wa kila mwaka (%) | | | | | | | | | | | | | |
| Jumla ya Fedha Taslimu | 9.0 | 12.2 | 17.0 | 12.2 | 5.5 | 3.9 | 0.9 | 7.6 | 3.7 | 9.8 | 8.0 | 10.3 | 6.4 |
| Wastani wa Fedha Taslimu | 8.0 | 9.6 | 8.1 | 9.2 | 4.6 | 6.1 | 3.3 | 2.7 | 7.4 | 6.0 | 10.0 | 12.0 | 9.5 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 17.2 | 17.5 | 18.8 | 21.3 | 17.4 | 14.5 | 12.4 | 13.7 | 14.1 | 12.8 | 13.1 | 13.8 | 10.9 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 15.6 | 17.8 | 18.0 | 18.2 | 15.9 | 14.0 | 12.2 | 11.8 | 11.9 | 11.1 | 11.0 | 11.9 | 8.9 |
| Mikopo kwa  Sekta Binafsi | 22.5 | 22.5 | 21.3 | 20.8 | 21.0 | 19.5 | 17.9 | 18.3 | 17.1 | 17.7 | 16.8 | 16.8 | 17.6 |

*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali 6: Riba za Masoko ya Fedha na Mitaji

*Asilimia*

| Aina ya riba | Apr-23 | May-23 | Jun-23 | Jul-23 | Aug-23 | Sep-23 | Oct-23 | Nov-23 | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (Overnight) | 4.12 | 3.25 | 3.92 | 3.94 | 4.35 | 4.64 | 5.36 | 5.70 | 6.56 | 6.75 | 6.35 | 6.20 | 6.51 |
| Siku 2-7 | 4.88 | 5.11 | 5.28 | 5.13 | 5.36 | 5.50 | 6.00 | 6.46 | 6.89 | 7.29 | 7.20 | 7.17 | 7.04 |
| Riba ya jumla | 4.92 | 5.02 | 5.25 | 5.06 | 5.24 | 5.46 | 5.90 | 6.36 | 6.81 | 7.27 | 7.20 | 7.10 | 7.02 |
| Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na Benki Kuu (Lombard rate) | 6.18 | 4.87 | 5.89 | 5.91 | 6.53 | 6.96 | 8.04 | 8.55 | 9.84 | 7.50 | 7.50 | 7.50 | 8.00 |
| Riba ya mikataba ya mauziano ya dhamana za muda mfupi (REPO rate) | 2.82 | 2.96 | 2.80 | 2.70 | 2.91 | 2.43 | 2.43 | 2.43 | 2.43 | 2.43 | 2.43 | 5.30 | 5.30 |
| Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 182 | 5.00 | 5.20 | 5.80 | 5.89 | 6.84 | 7.15 | 7.56 | 8.73 | 9.40 | 9.30 | 8.93 | 8.61 | 8.45 |
| Siku 364 | 6.72 | 6.98 | 7.14 | 7.02 | 7.03 | 7.72 | 8.73 | 9.49 | 10.51 | 11.81 | 12.25 | 11.82 | 10.38 |
| Riba ya jumla | 6.65 | 6.65 | 6.48 | 6.56 | 6.92 | 7.44 | 8.43 | 9.34 | 10.48 | 11.76 | 12.21 | 11.65 | 10.33 |
| Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 9.13 | 9.13 | 9.13 | 9.53 | 9.53 | 9.59 | 9.59 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 |
| Miaka mitano | 9.67 | 9.85 | 9.85 | 9.85 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 11.05 | 11.22 | 11.22 | 11.22 | 11.51 | 11.51 | 11.88 | 11.88 | 11.85 | 12.03 | 12.03 | 12.03 | 12.30 |
| Miaka kumi na tano | 11.63 | 11.63 | 11.96 | 11.96 | 11.96 | 12.34 | 12.34 | 12.34 | 12.75 | 12.75 | 13.66 | 13.66 | 13.66 |
| Miaka ishirini | 12.85 | 12.85 | 13.08 | 13.08 | 13.08 | 13.08 | 13.08 | 13.51 | 13.51 | 13.51 | 15.83 | 15.51 | 15.24 |
| Miaka ishirini na tano | 13.01 | 13.23 | 13.60 | 13.60 | 13.81 | 13.81 | 13.81 | 13.81 | 14.39 | 14.39 | 14.39 | 16.79 | 16.13 |
| Riba ya Benki Kuu | | | | | | | | | | 5.50 | 5.50 | 5.50 | 6.00 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

# Jedwali 7: Riba za Mabenki

*Asilimia*

| Aina ya riba | Apr-23 | May-23 | Jun-23 | Jul-23 | Aug-23 | Sep-23 | Oct-23 | Nov-23 | Dec-23 | Jan-24 | Feb-24 | Mar-24 | Apr-24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A: Shilingi ya Tanzania | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | 1.60 | 1.60 | 1.66 | 1.68 | 1.68 | 1.69 | 2.45 | 2.56 | 2.60 | 2.69 | 2.54 | 2.70 | 2.79 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 6.79 | 6.91 | 7.08 | 6.85 | 6.91 | 6.85 | 7.05 | 7.64 | 7.45 | 7.40 | 7.39 | 7.55 | 7.44 |
| Miezi sita | 8.22 | 7.49 | 7.72 | 7.90 | 8.08 | 7.95 | 7.66 | 8.46 | 9.14 | 9.13 | 9.07 | 9.15 | 9.12 |
| Mwaka mmoja | 7.70 | 8.34 | 8.68 | 8.70 | 8.93 | 8.98 | 9.00 | 9.16 | 8.92 | 9.15 | 9.06 | 8.94 | 8.21 |
| Riba za amana za wateja wakubwa | 9.46 | 9.24 | 8.82 | 9.08 | 9.04 | 9.29 | 9.24 | 9.15 | 9.19 | 9.56 | 9.52 | 9.59 | 9.33 |
| Riba za mikopo za Jumla | 15.91 | 15.96 | 16.02 | 15.56 | 15.73 | 15.53 | 15.49 | 15.38 | 15.44 | 15.39 | 15.44 | 15.51 | 15.42 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 16.55 | 16.60 | 17.10 | 16.30 | 17.01 | 16.07 | 15.93 | 15.63 | 15.94 | 15.82 | 16.10 | 16.17 | 15.93 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 17.24 | 17.36 | 17.17 | 16.92 | 16.99 | 16.87 | 16.75 | 16.91 | 15.91 | 15.82 | 15.71 | 15.74 | 15.77 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 15.92 | 16.11 | 15.99 | 14.79 | 14.59 | 14.86 | 14.98 | 14.90 | 15.82 | 15.92 | 15.80 | 16.05 | 15.87 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 15.57 | 15.54 | 15.68 | 15.61 | 15.68 | 15.59 | 15.67 | 15.45 | 15.48 | 15.39 | 15.51 | 15.42 | 15.44 |
| Riba za mikopo za wateja wakubwa | 13.65 | 13.02 | 13.11 | 13.19 | 13.31 | 13.37 | 13.26 | 13.29 | 13.38 | 13.44 | 13.40 | 13.46 | 13.95 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.08 | 0.07 | 0.05 | 0.04 | 0.04 | 0.00 | 0.01 | 0.02 | 0.04 | 0.04 | 0.04 | 0.91 | 0.79 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 3.10 | 3.28 | 3.34 | 3.43 | 3.75 | 3.51 | 3.67 | 3.78 | 3.67 | 3.40 | 3.73 | 3.82 | 3.77 |
| Miezi sita | 3.75 | 3.70 | 3.78 | 3.81 | 3.90 | 2.55 | 3.69 | 3.65 | 3.95 | 3.41 | 3.65 | 3.88 | 4.39 |
| Mwaka mmoja | 3.59 | 3.03 | 3.44 | 3.28 | 4.08 | 4.24 | 4.18 | 4.47 | 4.43 | 4.58 | 4.47 | 4.64 | 4.49 |
| Riba za mikopo za Jumla | 7.33 | 7.46 | 7.77 | 7.89 | 7.82 | 8.11 | 7.71 | 7.82 | 7.64 | 7.72 | 8.13 | 8.17 | 8.10 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 9.06 | 9.25 | 9.16 | 9.51 | 9.53 | 9.58 | 9.69 | 9.08 | 8.93 | 9.46 | 9.11 | 9.60 | 8.74 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 5.18 | 5.41 | 6.92 | 7.06 | 6.91 | 7.45 | 7.08 | 6.99 | 7.04 | 6.90 | 7.71 | 7.77 | 7.94 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 7.40 | 7.53 | 7.68 | 8.12 | 7.64 | 8.00 | 8.05 | 8.21 | 8.21 | 8.14 | 8.44 | 8.35 | 8.47 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 7.67 | 7.86 | 7.46 | 6.44 | 6.57 | 7.05 | 6.26 | 7.28 | 6.53 | 6.67 | 7.09 | 6.49 | 6.94 |

*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania*

# Jedwali 8: Bei ya bidhaa katika soko la dunia

| Bidhaa zitokanazo na Mafuta ya Petroli (Wastani wa USD wa kg) | Kahawa aina ya Arabica (USD/ kg) | Kahawa aina ya Robusta (USD/ kg) | Chai (Wastani wa USD/Kg) | Chai Mombasa (Wastani wa USD/Kg) | Mafuta ya Mawese (USD/tani) | Ngano (hard) (USD/tani) | Tumbaku (USD/tani) | Pamba (USD/kg) | Mbolea aina ya DAP (USD/tani) | Mbolea aina ya urea (USD/tani) | Dhahabu (USD/wakia) | Mahindi (USD/tani) | Mchele (USD/tani) | Sukari (USD/tani) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1,094.1 | 5.6 | 2.2 | 3.3 | 2.4 | 1,056.6 | 382.5 | 4,268.4 | 2.9 | 784.0 | 601.0 | 1,732.7 | 323.0 | 418.0 | 402.8 |
| 1,029.9 | 5.9 | 2.4 | 3.4 | 2.4 | 1,026.0 | 382.9 | 4,356.6 | 2.7 | 749.4 | 591.3 | 1,764.6 | 289.8 | 431.0 | 393.5 |
| 935.5 | 5.9 | 2.5 | 3.3 | 2.4 | 909.3 | 419.1 | 4,147.0 | 2.6 | 752.0 | 678.0 | 1,680.8 | 312.7 | 439.0 | 390.7 |
| 1,026.6 | 5.3 | 2.3 | 3.1 | 2.5 | 889.0 | 438.0 | 4,325.2 | 2.2 | 725.0 | 636.3 | 1,664.5 | 343.6 | 431.0 | 386.9 |
| 941.7 | 4.7 | 2.0 | 3.1 | 2.5 | 945.7 | 422.7 | 4,333.3 | 2.2 | 665.6 | 588.8 | 1,725.1 | 320.9 | 440.0 | 407.4 |
| 847.6 | 4.6 | 2.0 | 2.9 | 2.4 | 940.4 | 386.3 | 4,399.3 | 2.2 | 625.0 | 519.4 | 1,797.6 | 302.2 | 467.0 | 417.3 |
| 908.9 | 4.6 | 2.1 | 2.8 | 2.3 | 942.0 | 380.4 | 4,475.6 | 2.2 | 631.0 | 443.8 | 1,897.7 | 302.8 | 517.0 | 416.0 |
| 826.7 | 5.1 | 2.3 | 2.7 | 2.3 | 950.0 | 394.8 | 4,492.3 | 2.2 | 612.5 | 357.5 | 1,854.5 | 298.2 | 492.0 | 446.0 |
| 823.6 | 4.9 | 2.3 | 2.7 | 2.4 | 972.1 | 369.9 | 4,525.7 | 2.1 | 606.0 | 313.5 | 1,912.7 | 282.5 | 476.0 | 452.4 |
| 809.3 | 5.1 | 2.6 | 3.0 | 2.3 | 1,005.2 | 378.2 | 4,586.6 | 2.1 | 637.0 | 313.4 | 1,999.8 | 291.1 | 501.0 | 529.3 |
| 744.2 | 4.9 | 2.7 | 2.7 | 2.2 | 934.1 | 367.7 | 4,786.8 | 2.1 | 510.0 | 329.3 | 1,992.1 | 268.1 | 510.0 | 560.0 |
| 763.2 | 4.6 | 2.9 | 2.7 | 2.1 | 817.0 | 345.5 | 5,064.7 | 2.0 | 454.6 | 287.5 | 1,942.9 | 266.9 | 514.0 | 542.1 |
| 826.1 | 4.3 | 2.8 | 2.5 | 2.1 | 878.5 | 345.5 | 5,098.2 | 2.1 | 458.8 | 334.6 | 1,951.0 | 242.4 | 547.0 | 521.2 |
| 922.2 | 4.1 | 2.7 | 2.8 | 2.2 | 860.8 | 315.8 | 5,295.8 | 2.1 | 528.8 | 385.6 | 1,918.7 | 207.6 | 635.0 | 528.0 |
| 939.0 | 4.1 | 2.7 | 2.9 | 2.3 | 829.6 | 314.7 | 5,437.4 | 2.2 | 527.9 | 380.0 | 1,916.0 | 223.8 | 620.0 | 579.6 |
| 853.7 | 4.1 | 2.6 | 2.8 | 2.2 | 804.3 | 298.1 | 5,488.2 | 2.1 | 534.8 | 411.4 | 1,916.3 | 230.7 | 590.0 | 567.0 |
| 801.5 | 4.4 | 2.7 | 2.7 | 2.2 | 830.5 | 283.6 | 5,475.3 | 2.0 | 535.6 | 385.5 | 1,984.1 | 211.3 | 598.0 | 575.0 |
| 755.4 | 4.7 | 3.0 | 2.7 | 2.2 | 813.5 | 291.1 | 5,461.8 | 2.0 | 563.8 | 354.0 | 2,026.2 | 206.6 | 644.0 | 478.2 |
| 777.8 | 4.5 | 3.3 | 2.7 | 2.2 | 844.9 | 283.9 | 5,533.8 | 2.0 | 596.3 | 335.4 | 2,034.0 | 198.6 | 660.0 | 484.6 |
| 816.6 | 4.6 | 3.4 | 2.7 | 2.2 | 856.9 | 278.5 | 4,551.0 | 2.2 | 583.8 | 351.3 | 2,023.2 | 189.1 | 624.0 | 501.6 |
| 833.8 | 4.6 | 3.7 | 2.7 | 2.2 | 942.9 | 274.8 | 4,558.8 | 2.2 | 617.5 | 330.0 | 2,158.0 | 190.6 | 613.0 | 475.1 |
| 840.3 | 5.3 | 4.2 | 3.0 | 2.3 | 935.7 | 227.8 | 4,614.1 | 2.0 | 545.0 | 320.0 | 2,331.5 | 191.7 | 592.0 | 451.9 |

*Chanzo : http://www.worldbank.org/prospects*

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, 16 Jakaya Kikwete Road 40184,
Sanduku la posta 2303, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 22 223 2501/3022
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz